Revise & Assess Grade 7 Kiswahili - Majibu

1. **Kusikiliza na kuzungumza**

   Shughuli ya 1: Kusikiliza na kujibu mazungumzo

   1. Kusikiliza na kujibu mazungumzo kunahusu mtu kuhusika katika uzungumzaji na mtu mwingine au kundi la watu, ambapo anasikiliza kwa makini kisha anasema yake.
   2. (a) vipengele vya usikilizaji mazungumzo
      - Kusikiliza kwa makini
      - Kutomkata kauli mwenzio anapozungumza
      - Kutofanya mambo mengine unapozungumzwa
      - Kumwangalia anayezungumza

      (b) vipengele vya kujibu mazungumzo
      - Kumwangalia unayemjibu
      - Jibu tu kile umeulizwa kulingana na mazungumzo
      - Kuzingatia muktadha wa mazungumzo
      - Kutumia lugha inayofaa
      - Kuzingatia cheo na heshima ya unayemjibu

      (c) soma vipengele zaidi katika sehemu ya 'kumbuka'.

   3. Amtazame mgeni usoni kuona viziada lugha
      Anakili hoja muhimu
      Amsikilize mgeni kwa makini
      Ajiepushe na vitu vinavyoweza kuvuruga usikivu wake

   4. Zungumzia mwenzako, zingatia vipengele ulivyopewa.
   5. Andaa mazungumzo ya simu, pamoja na mwenzako, kuhusu usafi wa kibinafsi. Tumia vipengele vya kusikiliza na kujibu mazungumzo mlivyovisoma.

Shughuli ya 2: Kusikiliza kwa kina

1. (a) Kusikiliza kwa kina ni kuweka umakinifu wote kwa kile unachokisikiliza.
   (b) Umuhimu wa kusikiliza kwa kina:
   Ili kupata ujumbe kamili, ili kufahamu maana inayokusudiwa, ili kuepuka kutaka habari irudiwe, ili kuweza kujibu maswali kwa usahihi.

2. (a) Sauti **dh**: dha, dhi
   Sauti **th**: tha, tho
   (b) Sauti **dh**: dhana, ardhi, dhamani, maradhi, dhahabu, fedha, hafidhi, hodhi na taadhima.
   Sauti **th**: methali, theluji, theluthi, thamini, thurea na hadithi.
   (c) Sauti **dh**: radhi, maudhui, dhima.
   Sauti **th**: themometa, themanini, rithi.

3. (a) Tamka silabi ukizingatia matamshi sahihi ya sauti **dh** na **th**.
   (b) Sikiliza mwenzako akitamka maneno hayo.
   (c) Tamkia mwenzako maneno yenye sauti **dh**.

(d) Tamkia mwenzako maneno yenye sauti **th**.

4. Tamka maneno hayo, zingatia matamshi sahihi ya sauti **dh** na **th**.
5. Sikiliza mwenzako akikutamkia maneno yenye sauti **dh** na **th**, kisha mtajie maneno yenye sauti **dh** na yale yenye sauti **th** kati ya yale aliyokutamkia.
6. Muulize mwenzako akusomee kifungu. Mtathmini iwapo alitamka maneno yenye sauti **dh** na **th** kwa usahihi. Nawe, tamka maneno yenye sauti **dh** na **th** kutoka kwenye kifungu hicho.
7. (a) Tamka jozi za maneno hayo. Zingatia matamshi bora ya sauti dh na th.
   (b) Tunga sentensi kwa kila jozi ya maneno katika (a), ili kuonyesha tofauti ya maneno hayo. Umepewa mfano.
   (c) Wasomee wenzako sentensi hizo.

8. Tamka vitanzandimi huku ukizingatia matamshi bora ya sauti **dh** na **th**.
9. Unda vitanzandimi vitatu ukitumia sauti **dh** na **th**, vitamke kisha uwatamkie wenzako wakutolee maoni. Fuata mifano katika zoezi la 8.

Shughuli ya 3: Tanzu za fasihi

1. (a) Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu na kwa ufasaha katika kuwasilisha ujumbe.
   (b) Tanzu za fasihi ni: fasihi andishi na fasihi simulizi.
   (c) Soma maana ya fasihi andishi na simulizi katika sehemu ya ‘kumbuka’.

2. (a) Soma sifa za fasihi ulizopewa.
   (b)

Fasihi andishi	**Fasihi simulizi**
Huwasilishwa kwa maandishi.	Huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
Ni mali ya mtu binafsi.	Ni mali ya jamii nzima.
Ina tungo chache.	Ina tungo nyingi sana.
Huwa vigumu kubadilika kwani ikiandikwa husalia vilevile.	Inaweza kubadilika kutegemea. anayewasilisha na anayewasilishiwa.
Inaweza kuwasilishwa wakati wowote.	Ina wakati maalumu wa kuwasilishwa.

   (c) Soma sifa hizo ukiwa na mwenzako, kila mmoja safu yake.
   (d) Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi ni jinsi ilivyobainishwa katika (b) hapo juu na katika sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 7.
   (e) Jadili na mwenzako, mnaweza kufanya utafiti.

3. (a) (i) Tungo za fasihi simulizi: nyimbo, ushairi simulizi, maigizo, ngano, hadithi, vitendawili na methali.
   (ii)Sifa za tungo hizo hutokana na jinsi ya kuwasilishwa, wakati wa kuwasilishwa, nani fanani, nani hadhira na wahusika.
   (b) (i) Tungo za fasihi andishi: riwaya, novela, tamthilia na hadithi fupi.
   (ii)Sifa za tungo hizi hutokana na urefu, jinsi ya kuwasilishwa, idadi ya wahusika na wakati wa matukio.
   (c) Tungo za fasihi simulizi: hadithi, nyimbo, maigizo, semi, mazungumzo, ushairi simulizi.

Tungo za fasihi andishi: riwaya, tamthilia, ushairi, novela na hadithi fupi.

4. Fikiria utungo wa fasihi simulizi uuwasilishie wenzako.
5. (a)Kariri shairi hilo.
   (b) Shairi ni utungo wa fasihi andishi.
   (c) Sifa za ushairi: lina vina, beti, mishororo, ujumbe na wahusika.

Shughuli ya 4: Nyimbo za watoto na bembelezi

I. Nyimbo za Watoto

1. (a) Aina za nyimbo: nyimbo za watoto, bembelezi, nyimbo za mazishi (mbolezi), nyimbo za kidini, nyimbo za kisiasa na nyimbo za mapenzi.
   (b) Nyimbo za watoto ni nyimbo zinazoimbwa na watoto wakati wanapocheza.
   (c) Watoto
   (d) Wakati watoto wanapocheza
2. Sifa za nyimbo za watoto: huwa fupi, hurudiarudia sehemu, huandamana na vitendo au maigizo, huimbwa na watoto wanapocheza, huwa na mafunzo fulani kwa watoto, hubadilikabadilika kulingana na wakati au msimu, hutumia lugha rahisi.
3. (a) Vitendo vinavyoambatana na nyimbo za watoto: kucheza, kuruka, kujificha, kuigiza,kuhesabu nambari, kuhesabu miezi na siku.
   (b) Mitindo ya uwasilishaji nyimbo za watoto ni kama vile: kuimba wakiruka kamba, kukimbia na kujificha, kuchanganya ndimi, kurudiarudia vifungu.
4. (a) Waongoze wenzako kuimba wimbo huo.
   (b) Wakuambie iwapo umezingatia mitindo ya uwasilishaji mliyojifunza.
   (c) Wasilisha nyimbo nyingine za watoto uzijuazo ukizingatia mitindo ifaayo.
5. (a)Tunga wimbo wa watoto.
   (b) Wasilisha wimbo huo darasani kwa kuzingatia mitindo mwafaka.

II. Bembelezi

1. (a) Bembelezi ni nyimbo zinazoimbwa na mlezi wa mtoto kwa mtoto ili kumbembeleza alale au aache kulia.
   (b) Huimbwa na mlezi wa mtoto.
   (c) Huimbiwa mtoto ili alale au anyamaze anapolia.
2. Tafiti sifa za bembelezi kisha soma sifa katika sehemu ya ‘kumbuka’.
3. (a) Vitendo vinavyoambatana na bembelezi: kuimba, kupapasa mtoto, kurusharusha mtoto, kutembeatembea na mtoto, kumsifu mtoto.
   (b) Mitindo ya kuwasilisha bembelezi: Soma sehemu ya ‘kumbuka’ katika zoezi la 2.
4. (a) Imbia mwenzako wimbo huo.
   (b) Muulize akuambie iwapo umezingatia mitindo ifaayo.
5. Fanya zoezi hilo darasani.
6. (a) Tunga bembelezi fupi.
   (b) Wasilisha kwa wenzako kwa kuzingatia mitindo ifaayo.

Shughuli ya 5: Mazungumzo mahususi

1. (a) Soma maana ya mazungumzo mahususi katika sehemu ya kiangaza.
   (b) Maamkuzi: Unaendeleaje?, Waambaje?, U hali gani?, Hujambo?,
   Maagano: alamsiki, kwaheri, shinda salama, baki salama, wasalimie wote, buriani.

2. (a) Anamsikitikia mke wa Jomba kwa kumbeba mtoto pamoja na mizigo mingi ilhali mumewe anatembea tu!
   (b) Maamkuzi: Masalkheri!, Habari za siku nyingi?, Hujambo?, Sijui wewe!
   (c) Maagano: Fikeni salama, Kwaheri,
   (d) Majibu ya maamkuzi na maagano: akheri, njema, sijambo, salama, kwaheri ya kuonana.
   (e) Nyakati: Hujambo? – wakati wowote, masalkheri – jioni, Habari za siku nyingi? – wakati wowote, fikeni salama – wakati wowote, kwaheri – wakati wowote.

3.

Maamkuzi au maagano	**Jibu la maamkuzi au maagano**	**Wakati wa maamkuzi au maagano hayo**
Chewa!	Chewa.	asubuhi
Shikamoo!	Marahaba.	wakati wowote
Hujambo?	Sijambo.	wakati wowote
Sabalkheri	Sabalkheri/Akheri.	asubuhi
Habari/Habari yako	Njema.	wakati wowote
Waambaje?	Sina la kuamba.	wakati wwote
Umeshindaje?	Nimeshinda salama.	jioni
Kwaheri	ya kuonana	wakati wowote
Buriani	Buriani dawa.	wakati wowote
Alamsiki	Binuru.	jioni/usiku
Kwema?Habari za kwako?	Kwema.	wakati wowote
Makiwa	tunayo/yamepita asante tunayo/asante yamepita	wakati wowote kunapokuwa na msiba

4. (a)(i) Shikamoo babu! (ii) Hujambo mwalimu? Shikamoo mwalimu! (iii) Hujambo? (iv) Hamjambo? (v) Umeshindaje?
(b) (i) Marahaba (ii) Sijambo/Marahaba (iii) Sijambo (iv) Hatujambo (v) Nimeshinda salama.
5. (a) Nawe nenda salama (b) Binuru (c)ya kuonana (d)Nawe pia (e) Pia nawe.
6. (a)

Wakati		Maamkuzi	Majibu ya maamkuzi
(i)	asubuhi	Umeamkaje? Hujambo? Chewa!	Nimeamka salama/Sijambo/Chewa
(ii)	mchana	Habari za mchana/U hali gani?	Nzuri/Njema
(iii)	jioni	Masalkheri/Alamsiki/Umeshindaje/	Akheri/Binuru/Salama
(iv)	usiku	Lala unono/Alamsiki	Pia nawe/Binuru

(b)

Maelezo		**Maagano**	**Majibu ya maagano**
(i)	Mama kwa mtoto wake usiku	Alamsiki	Binuru.
(ii)	Mgeni kwa mwenyeji asubuhi	Shinda salama	Pia nawe.

(iii)	Mke kwa mume wake anayesafiri	Safiri salama	Nawe baki salama.
(iv)	Mhubiri kwa mgonjwa hospitalini	Ugua pole	Ahsante, nimepoa.

7. (a) Hujambo? (b) Baki salama (c) Habari za mchana ? (d) Umeshindaje? (e) Muwe na siku njema.
8. Shiriki maigizo hayo.

Shughuli ya 6: Kusikiliza kwa kufasiri: Matini

1. (a) Soma maana ya kusikiliza kwa kufasiri katika sehemu ya kiangaza.
   (b) Mambo ya kuzingatia katika kusikiliza kwa kufasiri: kusikiliza kwa makini, kutambua toni ya mzungumzaji, kutabiri kwa kuelekezwa na picha, kutambua maana ya msamiati unaotumiwa na kuzingatia mada inayozungumziwa.

2. Tabirianeni kuhusu kisa kwenye picha.
3. (a) Linganisha utabiri wenu na kisa chenyewe.
   (b) Kisa cha Maria kuumia kutokana na sakafu telezi.
   (c) Utelezi uliosababishwa na sakafu kutokaushwa vizuri.
   (d) Angepelekwa kwa kituo cha matibabu.
   (e) (i)kamsa – mayowe
   (ii) huduma ya kwanza – huduma ya kupunguza maumivu kabla ya kuhudumiwa na daktari
   (iii) utelezi – hali ya kuteleza kutokana na majimaji sakafuni

4. Kwa majibu ya zoezi hili, soma sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 17.

Shughuli ya 7: Kusikiliza kwa ufahamu

1. (a) Soma maana ya kusikiliza kwa ufahamu katika sehemu ya kiangaza.
   (b) Mambo ya kuzingatia katika kusikiliza kwa ufahamu: soma sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 18.

2. (a) Alifunga bao la kusawazisha.
   (b) Timu ya Tawaza kukosa huduma za mchezaji wao wa kutegemewa, Terry Ntinyari aliumia timu yake ikicheza na timu ya Zimwa, katika pambano hilo timu hizo zilitoka sare, timu ya Zimwa ilitangulia kufunga, Terry ndiye alifunga bao la kusawazisha, Terry alipoumia alipewa huduma ya kwanza kabla ya kupelekwa hospitalini.
   (c) ili kufafanua ujumbe katika (b), eleza kila hoja zaidi.
   (d) (i) mahiri – shupavu (ii) muundi – sehemu ya mbele ya mguu kati ya goti na wayo (iii) mchuano – mechi, shindano (iv) majeruhi – aliyeumia (v) akijigaragaza – akijirusharusha akiwa chini
   (e) (i) kwa mashobo – kwa maringo/mikogo (ii) kutangulia sio kufika – wa nyuma anaweza kushinda wa mbele (iii) kufyatua kombora – kupiga mkwaju mkali (iv) aliutumbukiza mpira kimiani – alifunga bao (v) walimpa huduma – walishughulikia hali yake.

Shughuli ya 8: Mazungumzo ya kupasha habari

1. Mazungumzo ya kupasha habari ni yale ambayo hufanyika kwa nia ya kufikisha ujumbe fulani. Kwa mfano, mazungumzo ya mafunzo kuhusu jinsi ya kujikinga na maradhi fulani, baraza la chifu, mazungumzo kuhusu mtaala mpya wa elimu n.k.
2. Mazungumzo ya kupasha habari:
   (a), (c), (d), (f), (g), (h).

3. (a) Hadhira imefahamishwa mengi kuhusu ulanguzi wa binadamu kama vile maana yake, wahusika na mbinu wanazotumia.
   (b) Maelezo kuhusu ulanguzi wa binadamu.
   (c) Vipengele vya mazungumzo ya kupasha habari viko katika sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 22.

4. Umuhimu wa kuzingatia vipengele vifuatavvo:
   a) Kuteua mada sahii – ili kupata ujumbe wa kupitisha
   b) Kuzingatia ukweli wa masuala – ili kupasha habari zisizo za uwongo.
   c) Kutumia lugha inayolinhana na hadhira – ili hadhira ielewe ujumbe kwa urahisi.

Shughuli ya 9: Kusikiliza kwa kina – sauti d na nd

1. Tamkia mwenzako maneno kama vile: dada, ndama, doli, ndio, dira na ndondi.
2. Kwa majibu ya swali hili, soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 23.
3. Sauti **d**: da, du, sauti **nd**: nda, nde.
4. Sauti **d**: doa, dodo, dua, kodi, duma, dada, dezo, dividii, dalia, jadili.
   Sauti **nd**: ndoa, mahindi, ndondi, mhundi, kikundi, ndimi, gundua, ganda, pinda.

5. Tamka silabi kwa usahihi, kisha msikilize mwenzako akitamka maneno umweleze iwapo ameyatamka kwa usahihi.
6. Tamka jozi hizo za maneno kwa usahihi ili kutofautisha sauti **d** na **nd**.
7. Fanya utafiti kisha utamke kisahihi maneno yenye sauti ulizoagizwa
8. Fanya zoezi hili kulingana na maagizo.

Shughuli ya 10: Nyimbo za kazi na dini

I. Nyimbo za kazi (Hodiya)

1. (a)Nyimbo za kazi ni nyimbo zinazoimbwa na wanajamii wanapofanya shughuli mbalimbali.
   (b) Huimbwa katika mazingira ya kufanya kazi.
   (c) Huwa na ujumbe wa kutia moyo watu kuendelea na kazi.
2. (a) Wimbo wa kazi, unahimiza watu kufanya kazi ya ukulima.
   (b) Huimbwa shambani.
   (c) Unahimiza watu kushika jembe na kulima bila kuogopa kuchafuka, ndipo wapate chakula na kufukuza njaa.
   (d) Maigizo ya kushika jembe, kukunja uso kuonyesha kuchoka, kutikisa kichwa kusisitiza kushika jembe sawasawa.

3. Fanya zoezi hili kulingana na maagizo. Elekezwa na majibu ya zoezi la 2 hapo juu.

II Nyimbo za dini

1. (a) Nyimbo za dini ni nyimbo zinazoimbwa wakati wa kuabudu Mungu.
   (b) Huimbwa katika sehemu za kuabudia.
   (c) Huwa na ujumbe wa kumsifu Mungu, kuwapa waumini matumaini, kutangaza wokovu, kuwasihi watu kuacha dhambi na mengineyo.
2. (a) Wimbo wa dini, unamsifu muumba.
   (b) Sehemu za kuabudia kama vile makanisani.
   (c) Unamsifu Mungu, unawaita wote kumsifu kwa kucheza vyombo mbalimbali, unainua jina la mwenye kutoa uhai.
   (d) Kupiga makofi,kuchezesha mwili upande na upande,ishara za uso za kudhihirisha furaha(kutabasamu)

3. Fanya zoezi hili kulingana na maagizo.
   Shughuli jumuishi
   Tafiti ili kujibu zoezi hili. Elekezwa na zoezi la 1 na la 2 hapo juu.

Shughuli ya 11: Kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara

1. Kwa majibu ya zoezi hili, soma kiangaza na sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 27.
2. (a) Kutabasamu, kucheka, kupiga makofi, kusimama, kuashiria kwa mkono, kuweka kidole kwa mdomo, kukuna kichwa,kutikisa kichwa.
   (b) Ishara na vitendo hivyo vimesaidia katika kupitisha ujumbe, kwa mfano kuweka kidole kwa mdomo kulinyamazisha wanafunzi, kukuna kichwa kunaonyesha kufikiria.

3. Ishara zihusiane na vitendo husika.
4. Tafiti ili kujibu zoezi hili.

Shughuli ya 12: Kusikiliza kwa makini

1. Kwa majibu ya zoezi hili, soma kiangaza katika uk wa 29 na sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 30.
2. (b) Kujiepusha na mambo mengine yoyote na kusikiliza tu, kumtazama msomaji, kutomkata msomaji, kuwa mtulivu.
   (c) Zamani magonjwa hayakuwa mengi, mababu walikuwa na suluhu kwa kila ugonjwa uliokuwapo, baadaye ukimwi ulizuka aidha kutokana na sokwe au maabara ya kisayansi, korona ilitetemesha dunia na kufanya watu kuogopa kutangamana.

Shughuli ya 13: Wahusika katika nyimbo

1. (a) Wahusika ni viumbe watumiwao na mtunzi kupitisha ujumbe katika kazi ya fasihi.
   (b) Ili kutambua mhusika katika wimbo, fuata anayetoa ujumbe na yule anayelengwa na ujumbe huo.
   (c) Wao ndio hupitisha ujumbe wa wimbo.
   (d) Sifa zitatokana na maneno na matendo ya wahusika.

2. (a) Marafiki-smwimbaji na anayeimbiwa.
   (b) Mwimbaji: mwenye mapenzi ya dhati kwa rafikiye, anathamini urafiki, mwenye shukrani,anayeamini (mcha)Mungu, msamehev na mwenye matumaini.
   Anayeimbiwa: mwenye utu,msaliti, kigeugeu(asiye na msimamo), asiyethamini urafiki, mnyanyasaji na msamehevu.
   (c) Umuhimu wa kusameheana, hakuna haja kulipiza kisasi, marafiki hukosana na kupatana,umuhimu wa kusaidiana katika dhiki.
   (d) Anampenda na kumuamini japo yeye hamthamini.
   (e) Kutoaminiana, kutothaminiana,kubadilisha mienendo.
   (f) Wamesameheana na kupatana.
   (g) Watu hukosana na kupatana tena wanaposameheana.

Shughuli ya 14: Lugha katika nyimbo

1. (a) Nyimbo hutumia fani mbalimbali za lugha kuwasilisha ujumbe, kwa mfano methali, semi na nahau.
   (b) soma jibu la swali hili katika sehemu ya 'kumbuka' uk wa 33.

2. (a) Pesa (b) Ametumia uradidi(takriri), tashihisi, tashbihi na chuku. (c) majibu ni kama (b). (d) kuongeza chumvi au utamu katika maelezo, kusisitiza ujumbe, kuficha ujumbe.
3.

Kipengele cha lugha	**Umuhimu**
(i) Methali	Kuunda uhusiano kati ya hali fulani na nyingine.
(ii) Tashbihi	Kulinganisha hali mbili kwa kutumia vilinganishi kama vile kama, sawa na, mfano wa, na mithili ya.
(iii) Urudiaji/Takriri/Uradidi	Kusisitiza ujumbe
(iv) Majazi	Kuunda taswira ya kipekee kwa kumpa mhusika, kukipa kitu au mahali jina kulingana na sifa,tabia, mienendo au hali yake.

4. (a) Nahau, istiari, semi na kinaya.

(b) Nahau – kumfikirisha mtu zaidi, istiari – kufananisha mtu, kitu au hali moja kwa moja, semi – kusisitiza ujumbe, kinaya – kuficha maana, kupunguza makali na kukejeli.

Shughuli ya 15: Kusikiliza habari na kujibu

1. Kwa majibu ya swali hili soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 35.
2. Utabiri: maelezo ya mtu mwenye maadili ni mtu wa aina gani, majibu yalingane na vidokezo.
3. (a) Kadiria
   (b) Maadili
   (c) Maana ya maadili, sifa za mtu mwenye maadili na madhara ya kukosa maadili katika nchi.

(d) Mwenendo, tabia, anayeaminika, mkweli, heshima, utovu wa maadili, kutunza wakati.
(e) Maana itokane na muktadha wa matumizi.

2. **Kusoma**

Shughuli ya 1:Ufahamu wa kifungu cha simulizi

1.(a) Tunasoma ufahamu ili :

(i) Kupata maarifa mapya.

(ii) Kukuza uwezo wa kufikiri.

(iii) Kujenga na kukuza mbinu za kuandika.

(iv)Kunoa uwezo wa mawasiliano

(v) Kukuza msamiati na stadi za lugha.

(vi)Kupata burudani.

(vii) Kuchochea na kukuza ubunifu.

b) Mambo yanayosaidia kuelewa vifungu vya ufahamu .

(i) Kuwa makini unaposoma kifungu cha ufahamu.

(ii) Kujaribu kukisia maana ya msamiati kulingana na muktadha .

(iii) Kujiuliza maswali ya kujitathmini kama vile kifungu hiki kinahusu nini ? Nimejifunza nini ?

(iv) Kusimulia kifungu kwa wengine .

(v) Kutafuta maana ya msamiati kwa kamusi .

2. Soma kifungu kwa kuzingatia mbinu za usomaji bora wa vifungu vya ufahamu .

3. (i) Lugha iliyotumika katika kifungu ni ya kawaida inayoeleweka kwa urahisi .

(ii) Matukio katika kifungu hiki yanafuatana moja kwa moja kwa mtindo sahili kuanzia mwanzo hadi mwisho .

(iii) Matukio ya ufahamu yanajitokeza kwa njia ya masimulizi .

(iv) Vitendo vya safina vinajenga matukio na kuelezwa kwa kina .

4.(a) - Alitandika kitanda chake kwa shuka safi .

- Aliweka shuka chafu kwenye kapu la nguo chafu .
- Alipiga meno mswaki na kunawa uso.

(b)

(i) kapu la nguo chafu

(ii)taulo

(iii)mswaki na dawa ya kupiga mswaki

(iv)Sabuni

(v) Kitana

(vi)Mafuta ya nywele

(vii)Vipodozi na sodo

(viii)Kabati

(ix)Mashine ya kuosha nguo

(c) Safina alitumia vifaa vifuatavyo kudumisha usafi:

(i) Maji

(ii) sabuni

(iii) mafuta

(iv) mswaki na dawa ya kupiga mswaki

(v)Vipodozi

(vi) Kitana

(vii) Sodo

(d) Aina za usafi wa kibinafsi zilizotajwa katika kifungu ni pamoja na :

(i) Usafi wa mwili - Safina alioga mwili wote na kutumia vipodozi . Pia alipiga meno

mswaki .
(ii) Usafi wa malazi-anatumia shuka safi kutandika kitanda chake .

(iii)Usafi wa mazingira - anapanga chumba chake vizuri pamoja na kabati

(iv)Usafi wa mavazi - anaosha nguo na shuka chafu .

(v) Usafi wa vyakula - anaosha matunda kabla ya kuyala .

5.Matukio yanafuatana ifuatavyo
c, e , b, a , d .

6(a) Safina hangeweza kushughulikia usafi wa nyumbani kama vile kupanga chumba chake na kuosha nguo zake chafu.

(b) Meno yake yangepoteza weupe wake na pia angenuka mdomo na kutengwa .

(c) Haingekuwa rahisi kuziosha nywele na kuzichana.
(d) Haingekuwa rahisi kuziosha kwa mikono na ingemlazimu kutumia mashine .
(e) Kucha hizo zingehifadhi uchafu ambao hubeba viini ambavyo vingemsababishia magonjwa .

7.(a)
(i) safi - isiyo na uchafu
(ii) taulo -kipande cha nguo maalum kinachotumiwa kufutia mwili baada ya kuoga
(iii) sabuni - kitu kinachotoa povu kinapochanganywa na maji na ambacho hutumiwa kutekeleza usafi .

(iv) kuzichana - kuzitengeneza nywele kwa kutumia kitana .

(v)chawa - mdudu anayeletwa na uchafu na ambaye hukaa kwenye nywele au nguo

chafu

(vi) Sodo - kifaa kinachotumiwa na wanawake kudumisha usafi wakati wa hedhi.

(b) Maana ya nahau

(i)kupiga mswaki-kusafisha meno kwa kuyasugua kwa dawa ya meno pamoja na maji

(ii)kupiga deki-kusafishsa sakafu

(iii)kushtaki njaa-kula

Shughuli ya 2. Kusoma kwa mapana : Matini ya kujichagulia.

1 (a) Matini mbalimbali kama vile matini ya kisayansi , burudani , kitaaluma zitajwe .

(b) Rejelea sehemu ya kumbuka uk 41- 42.

2. (a)Msamiati wa lishe bora uliotumika katika matini ni pamoja na:
(i) wanga (ii) virutubisho (iii) protini (iv) vitamini (v) mafuta (vi) kalori

(b) (i) wanga - chakula kinachompa mtu nguvu .

(ii) virutubisho - viini vinavyopatikana katika chakula na ambavyo ni muhimu kwa ukuaji wa viumbe
(iii) protini - thamani katika chakula ambayo husaidia kujenga mwili.
(iv) vitamini - virutubisho katika chakula ambavyo humpa mtu kinga dhidi ya magonjwa.

(v) mafuta - kitu kama maji ambavyo hupatikana katika aina fulani za matunda na wanyama kama samaki.
(vi) kalori - vipimo vya virutubisho mbalimbali vinavyohitajika mwilini

(c)(i) Lishe - chakula chenye virutubisho vyote muhimu .
(ii) virutubisho - viini katika chakula na ambavyo ni muhimu kwa ukuaji wa binadamu .

(iii)kalori - vipimo vya virutubisho mbalimbali vinavyohitajika mwilini

(iv) Kinga - uwezo wa mwili kupigana na magonjwa.

(v)Kisukari - ugonjwa ambao humpata mtu viwango vya sukari vikizidi au kupungua mwilini.

(vii)kudumaa - kutokua vizuri kwa binadamu kutokana na lishe isiyofaa .

(vi)saladi - matunda na mboga zilizokatwakatwa na kuliwa zikiwa mbichi .

(d) Sentensi zionyeshe matumizi yanayofaa ya msamiati husika .

(e)Lishe bora ni muhimu kwa ukuaji wa mwili na kuuwezesha mwili kupigana na magonjwa .

(f) Muhtasari ujumuishe hoja zifuatazo

(i) Lishe bora hujumuisha chakula chenye virutubisho muhimu ambavyo ni muhimu kwa ukuaji na kukinga mwili dhidi ya magonjwa .

(ii) Lishe bora husaidia ukuaji na ikikosekana madhara yake hujidhihirisha kwa njia mbalimbali kama vile magonjwa na kudumaa .

(iii) Lishe bora humsaidia binadamu kuwa na ngozi na nywele nzuri .

(iv) Ili kupata lishe bora chakula kiliwe bila kuruka mlo wowote , mara tatu kwa siku na kijumuishe matunda .

(v) Maji pia ni sehemu muhimu ya lishe bora .

(vi) Vitu ambavyo vinasisimua mwili viepukwe .

(g) Wasilisha uliyoyarekodi kwa wenzako.

Shughuli ya 3 Kusoma kwa kina : Novela

1. (a) Novela - Ni kisa cha kubuni kilichoandikwa kwa lugha ya nathari chenye urefu wa wastani.

(b) (i) Yaliyomo au maudhui - maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika novela . Katika novela maudhui huwa machache kuliko yale ya riwaya lakini mengi kuliko ya hadithi fupi .

(ii) Urefu - Novela huwa na urefu wa wastani kati ya kurasa 96- 100 . Huwa ndefu kuliko hadithi fupi lakini fupi kuliko riwaya .

(iii) Mtindo - hutumia mtindo usio changamano . Kwa mfano hakuna matumizi mengi ya mbinu rejeshi .
Kutakuwa na mbinu za kimtindo kama vile methali , nahau , misemo , chuku , tashihisi , taswira , kejeli , kinaya n.k

(v) Ploti - novela huwa na ploti sahili . Matukio hufuatana moja kwa moja bila matumizi ya mbinu rejeshi .

(vi) Wahusika - wahusika huwa si wengi sana kama katika riwaya . Wahusika wakuu huwa wachache na mwandishi hana nafasi kubwa sana ya kuwakuza .

(vi) Matukio - matukio ya novela huwa si mengi kama vile katika riwaya .

2. Sifa zinazoafiki novela ni a,d,f,h na i.

3.(a) Urefu - urefu ni wa wastani .Huwa na kati ya kurasa 96- 100
(b) Ploti - huwa na ploti sahili ambapo matukio hufuatana moja kwa moja bila matumizi ya mbinu rejeshi .

(c) Lugha - si changamano . Huwa sahili .

(d) Maudhui - maudhui huwa machache .

(e) Mandhari - mandhari huwa si changamano . Yanajitokeza waziwazi .

(f) Wahusika - huwa wachache kuliko wale wa riwaya na huwa hawajakuzwa kikamilifu

3. Mwanafunzi baada ya kusoma novela atambue sifa kama vile:
(a) Ina urefu wa wastani
(b)Ploti yake huwa sahili
(c)Hutumia lugha ya nathari kueleza matukio
(d)Maudhui yake huwa machache
(e)Huwa na mandhari finyu
(f) Wahusika huwa wachache na wasiokuzwa kikamilifu .
(g)Haina migao ya sura

Shughuli ya 4: Kusoma kwa ufasaha

1 (a) Kusoma kwa ufasaha ni kusoma kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora.
(b)Vipengele hivi ni pamoja na utamkaji bora wa sauti na maneno , kuzingatia kasi inayofaa, sauti inayosikika na matumizi ya ishara zinazofaa .Pia matumizi ya toni na kiimbo kinachofaa huzingatiwa.
Vipengele vya kuzingatia katika kusoma kifungu kwa ufasaha vilingane na vile vilivyoorodheshwa katika sehemu ya **Kumbuka** uk 44 .

2 . (a) Mwanafunzi asome kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora.

(b) Maoni ya wanafunzi yajikite katika kumwelekeza mwenzao katika mbinu na vipengele vya usomaji bora wanafunzi.
(c)Rejelea vipengele vya usomaji bora katika 1.(b)

Shughuli ya 5 Kusoma kwa ufahamu : Kifungu cha ufahamu

1. Habari mahasusi zinazojitokeza katika kifungu hiki .

- Kuwa licha ya tofauti za kimaumbule zisizopingika kati ya wanaume na wanawake hakuna jinsia iliyo bora kuliko nyingine .
- Dhuluma kwa misingi ya jinsia haifai.

Kuwa bado zipo jamiii ambazo zinazingatia tamaduni zinazotenga majukumu katika jamii kwa misingi ya jinsia .

- Kuna ubaguzi wa kijinsia katika ajira ambapo watu hunyimwa kazi fulani kwa sababu ya jinsia zao.
- Usawa wa Kijinsia ni kigezo muhimu katika kuhakikisha ustawi wa nchi .
- Twafaa kupiga hatua kwa kupuuza mitazamo ya kale kuhusu jinsia .

Ufupisho

- Hatua za kuandika ufupisho kama zilivyoekezwa katika Uk 47- 48 zizingatiwe .
- Hoja zote muhimu zijumuishwe. Hizi ni pamoja na.
- Tofauti za kimaumbile kati ya mwanaume na mwanamke zi wazi na hasipingiki.
- Wanaume na wanawake wamepewa uwezo wa kutekeleza majukumu yoyote bila kujali jinsia .
- Ni dhuluma kuachia jinsia moja baadhi ya majukumu

-Zipo jamii ambazo zimetenga baadhi ya majukumu kwa jinsia fulani na kuona mwiko majukumu fulani kutekelezwa na jinsia fulani.

- Kuna ubaguzi katika ajira kwa misingi ya jinsia .
- Usawa wa kijinsia ni kigezo muhimu katika kuhakikisha usawa ustawi wa nchi .
- Ulimwengu wa sasa haufai kukubali ugawaji wa majukumu kwa misingi ya jinsia .

(c)

(i) Jinsia - hali ya kuwa mwanaume au mwanamke , uana

(ii) Ubaguzi - unyimaji wa watu kazi kwa misingi ya kijinsia .

(iii) Majukumu - wajibu wa mtu katika jamii. Mambo Yanayofaa kutekelezwa na mtu fulani

(iv) Ndwele - ugonjwa

2. a- f tekeleza shughuli zote .

Nje ya darasa

1. Tafuta kifungu mwafaka
2. (a) Habari muhimu zindondolewe.
   (b) Fupisha ujumbe kwa kuzingatia utaratibu bora wa ufupishaji.
   (c) Msomee mzazi au mlezi ufupisho wako.
   (d) Mweleze mlezi au mzazi maana ya msamiati kutoka kifungu hicho.

Shughuli ya 6 :Kusoma kwa kina:Maudhui na dhamira

1. Dhamira ni lengo la kazi fulani ya fasihi.
2. (a) Mwandishi alilenga kuonyesha matarajio ya wazazi kuhusu ya maendeleo ya watoto

wao.

(b) Mwandishi analenga kuonyesha matarajio ya jamii kuhusu maendeleo ya watoto kupitia masomo na jinsi jamii ilivyoenzi masomo ya watoto wa jinsia zote .

Aidha , mwandishi anaendelea kuonyesha umuhimu wa wazazi katika kuwaelekeza watoto wao katika njia zitazowafaa.

Mwandishi hata hivyo, pia anaonekana kulenga pia kuonyesha kuwa jitihada haiondoi kudura na liandikwalo ndilo liwalo kwani Zureya anakatiza masomo yake ghafla na kuamua kumfuata swahibu aliyeishi Mashariki ya Mbali kinyume na matarajio ya babake .

II

1. (a) Maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi
   (b) Shughuli itekelezwe

2 (a) Maudhui mbalimbali yanajitokeza yakiwemo :
(i) Kilimo - mzee Makini alikuwa mkulima . Alikuwa amepanda aina mbalimbali za matunda na mboga na kuwafuga wanyama na ndege mbalimbali .
(ii) Elimu - jamii hii ilithamini masomo ya mtoto msichana na tunaona Mzee Makini akifanya kila jitihada kumsomemesha mtoto wake Zureya .

(iii) Usawa wa jinsia katika masomo - Jamii alithamini masomo ya mtoto msichana .

(iv) Uwajibikaji - wazazi wanawajibika kutekeleza majukumu yao. Kwa mfano familia ya Bwana Makini inaonyesha uwajibikaji kwa kumsomesha mtoto wao Zureya .
(V) Malezi bora - Makini alimkumbusha bintiye kila siku umuhimu wa nidhamu katika maisha .

b) Muhtasari ulenge maudhui yaliyojadiliwa hapo juu .

Shughuli Jumuishi (a - f)
Tekeleza shughuli zote .

Nje ya darasa (1-3) Shughuli zote zitekelezwe

Shughuli ya 7 Ufupisho Uk. 51-52

1.(a) Ufupisho ni kueleza upya habari kwa maneno machache bila kupotosha ujumbe .

(b) Kifungu kina aya sita . Ujumbe katika kila aya unaweza kufupishwa ifuatavyo

1. Shule ya Huduma ilikuwa na furaha kupata nafasi ya kuwa mwenyeji wa Tamasha la muziki baada ya muda mrefu.
2. Mwalimu mkuu aliandaa mkutano wa viranja katika ukumbi wa mikutano.
3. Mwalimu mkuu Bi. Kerubo aliwaeleza viranja alichowaitia.
4. Wanafunzi wakiongozwa na viranja walifanya maandalizi kwa kuzingatia usafi shuleni kote.
5. Sehemu zote za shule ziling'arishwa.
6. Kiranja mkuu aliwajibika vilivyo katika kuongoza maandalizi ya siku hiyo ambayo waliitarajia kwa hamu sana.

(c) Ufupisho ujumuishe hoja zote zilizoorodheshwa katika *b* hapo juu na zikiwa zimeunganishwa kujenga aya .

(d) Wasilisha ufupisho uliouandika kwa wenzako kisha wautolee maoni.

2. (a- b) Tafuta matini ya kidijitali , uisome na uifupishe kwa kuzingatia hatua za ufupishaji zilizoorodheshwa katika sehemu ya **Kumbuka** hapo juu (uk 52)

Nje ya darasa (1-4) Shughuli zote zitekelezwe .

Shughuli ya 8 :Kusoma kwa kina : Mandhari na ploti

1. Mandhari katika fasihi hurejelea sehemu au mazingira ambamo matukio yanatendeka. Nayo ploti hurejelea jinsi matukio yalivyopangwa katika kazi ya fasihi kulingana na visababaishi vyake.

2. (a) Mambo yafuatayo huzingatiwa ili kutambua mandhari ya novela.

(i) Maelezo ya mwandishi kuhusu mahali wanamoishi wahusika . Aina za majengo n.k

(ii) Maneno ya wahusika wenyewe kuhusu hali zao za kiuchumi , kijamii n.k.

(iii) Kipindi / Muda - wahusika wanaishi katika kipindi gani cha kiwakati. Hili laweza kujitokeza kupitia maneno ya wahusika , maelezo ya mwandishi.

(iv) Muktadha wa kiuchumi na kijamii wa jamii inayohusika . Je wahusika wanaishi maisha ya aina gani ?

(v) Hisia za wahusika - zingatia hisia za mwandishi kuhusu hali na maisha ya wahusika. Pia hisia za wahusika wenyewe kuhusu maisha yao wenyewe yanaweza kudokeza aina ya mandhari .

(vi) Matendo ya wahusika -matendo ya wahusika yanaweza kumwelekeza msomaji kutambua mandhari . Kwa mfano ikiwa wahusika wanalala njaa, jambo hilo linaweza kuelekeza msomaji kuhusiana na hali ya kiuchumi ya wahusika.

(b) Tambua mandhari mbalimbali kama vile :

(i) Madhari ya kisiasa kama vile mifumo ya kisiasa , hali ya kisiasa katika jamii husika n.k

(ii) Mandhari ya kijamii kama vile hali ya masomo , miundo mbinu ya kijamii kama vile shule , hospitali n.k

(iii) Mandhari ya kiwakati / kihistoria

(iv) Mandhari ya kijiografia kama vile misitu , mito ,milima n.k

(d)Mandhari huwa na dhima ama umuhimu ufuatao katika fasihi:

(i) Husaidia kujenga na kukuza maudhui

(ii) Husaidia kuwasilisha dhamira na ujumbe

(iii)Huwezesha sifa za wahusika kujitokeza

(iv)Hukuza mivutano na migogoro katika hadithi

(v)Hukuza muktadha wa novela

(vi) Hutambulisha wahusika

(d) (i) Kuuza na kununua kama vile katika mandhari ya mjini

(ii) Shughuli kama vile kulima katika mandhari kama vile ya mashambani

(iii) Shughuli za masomo katika mandhari ya shuleni na vyuoni

(iv) Katika mandhari ya kiasili kama vile milima kutakuwa na shughuli kama vile kukwea milima n.k.

(v)Katika mandhari ya kisiasa kutakuwa na mambo kama vile kampeni na upigaji kura ukiendelea.

(e) Mandhari hufanikisha ujumbe kwa njia zifuatazo:

(i) Huleta uhalisia - kwa mfano uhalisia wa maudhui ya umaskini utaletwa na mandhari yenye makazi hafifu , watoto wanaovaa matambara n.k

(ii) Hukuza hisia zilizokusudiwa na mwandishi kwa mfano hisia za huruma , za furaha

(iii) Mandhari hufanikisha ujumbe kwa kubainisha muktadha uliokusudiwa

(iv) Huchochea wahusika kuchukua hatua

(v) Husaidia kujenga mtindo

(f) Shughuli itekelezwe.

3. (a) Ufisadi - Mandhari yataonyesha ufisadi kwa kuonyesha matukio kama vile

watu kupokea na kutoa hongo , wizi wa mali ya umma .
(b) Umaskini -utaonyeshwa na mandhari yanayoonyesha wahusika wakiishi kwa mfano katika makaazi hafifu kama vile nyumba za karatasi , watoto kuvaa matambara .
(c) Tofauti za kitabaka - wahusika mbalimbali watakuwa wakiishi maisha tofautitofauti kama vile wengine wakiishi maeneo ya kifahari wengine wakiishi kwa madongoporomoka , watoto wa matajiri wakisomea shule za kifahari wa maskini wakiishi shule zenye miundomsingi duni .
(d) Elimu - Kutakuwa na taasisi na shughuli za masomo katika mandhari hayo .

II Ploti

1 (a) Ploti hurejelea mfuatano au mtiririko wa matukio katika hadithi kulingana na visababishi vyake.

(b) Ploti huwa na vipengele vifuatavyo:

(i) Wahusika

(ii) Mandhari

(iii)Mtindo

(iv)Muktadha

(v)Mwanzo , kilele na hitimisho

2. (a) Kuna aina mbili za ploti
(i) Ploti sahili - ambapo matukio hufuatana moja kwa moja
(ii) Ploti changamano - ambapo matukio hayafuatani moja kwa moja

b) Ploti huwa na umuhimu ufuatao katika hadithi:

(i) Husaidia kukuza wahusika na sifa zao. Kwa mfano katika ploti changamano mwandishi anaweza mrudisha msomaji nyuma ili apate kuelewa maisha ya hapo awali ya mhusika.

(ii) Hukuza mgogoro wa hadithi na kupitia mgogoro huo ujumbe hujitokeza.

(iii) Husaidia kuchochea hisia mbalimbali ambazo huimarisha ujumbe .

(iv) Husaidia maamuzi ya wahusika na matokeo yake kujitokeza. Kupitia maamuzi

ya wahusika ujumbe huimarika.

Shughuli Jumuishi uk 54

1. Uhusiano kati ya dhana mbalimbali za fasihi .

(a) Mandhari na ujumbe-mandhari husaidia mwandishi kukuza hisia muhimu kwa kufanikisha ujumbe . Kwa mfano mandhari magumu ya kiuchumi yatafanya msomaji apate ujumbe kuhusu unyanyasaji , n.k

(b) Mandhari na wahusika – huwatambulisha wahusika na kusaidia sifa zao kujitokeza .

(c) Mandhari na ploti - mandhari husaidia kukuza mgogoro ambao ni muhimu kuendeleza matukio yanayojenga ploti .

(d) Ploti na ujumbe - ploti husaidia kuimarisha na kujitokeza vizuri kwa ujumbe .

(e) Mandhari na maudhui - mandhari mbalimbali husaidia kujenga maudhui mbalimbali . Kwa mfano mandhari yakitofautina sana yanaweza jenga maudhui ya utabaka n.k..

2 (a) Tazama maelezo ya ploti na mandhari katika uk 53 na 54(zingatia mapendekezo pambizoni kwenye matini)

Tazama aina mbalimbali za mandhari katika uk wa 53(zingatia mapendekezo yaliyotolewa uk 53)

(c) Zingatia umuhimu wa mandhari katika uk 54(zingatia mapendekezo pambizoni katika ukurasa huu) kisha kwa kutoa mifano katika novela uliyoisoma ueleze umuhimu wa mandhari katika riwaya hiyo .

(d) Kamilisha shughuli

(e) Kwa kurejelea novela uliyosoma tambua kama ploti ni sahili au changamano.

(f) Ukizingatia umuhimu wa ploti ulioelezwa katika uk wa 54(zingatia mapendekezo katika ukurasa huu kwenye matini),eleza kwa kutoa mifano umuhimu wa ploti katika novela uliyoisoma .

(g) Maelezo ya ploti yajumuishe aina ya ploti na mtiririko wa matukio .

(h) Wasilisha uchambuzi wako wa ploti na mandhari ya novela uliyoisoma kwa wenzako .

Nje ya darasa (1-2)

Shughuli itekelezwe kwa ukamilifu .

Shughuli ya 9 Ufahamu wa kifungu cha shawishi

1 (a) (i)Alikuwa akienda posta kutuma barua kwa ndugu yake anayeishi mjini .

(ii) Kumwona Boke akizungumza na mtu mwingine kwa njia ya video

(iii) (a)Hutumiwa kupiga picha na kurekodi video.
(b) Hutumiwa kuonyesha wakati na siku kwani zina saa na kalenda .

(c)Simu zina michezo ya burudani.

(d)Hutumika kuhifadhi habari na data muhimu.

(e) Hutumiwa kukokotoa hesabu mbalimbali.
(f)Hutumiwa kutuma na kupokea pesa.

(iv) Kite alikuwa na maoni hasi kuhusu simu. Kuwa simu hununuliwa kwa bei ghali na hutumia pesa nyingi kwa 'credit' .

(v) Alimfafanulia jinsi simu zilivyo nafuu kutegemea aina ya simu na jinsi zinavyowasilisha ujumbe kwa njia rahisi .
Pia alimpigia ndugu ya Kite simu na akapata kuongea naye kwa urahisi.

(b) Boke aliweza kumshawishi Kite kwa sababu Kite aliamua kununua simu na kuachana na safari yake ya kuenda posta .

(c) - simu
- video
- skrini

(d) Maana ya msamiati huu wa kidijitali

(i) Simu - kifaa kitumiwacho kuwezesha mawasiliano ya hewani kati ya watu walio mbalimbali .

*(ii) video - kifaa /" app" kwenye simu kinachowezesha watu wawili au zaidi kuwasiliana huku wakionana moja kwa moja .
Pia hutumiwa kunasia sauti ,picha hai na filamu.

(iii) skrini - kiwambo cha simu kinachoonyesha picha au maneno kinapotumika.

(e) (i) Posta - mahali ambapo barua hupokelewa na kusafirishwa

(ii) Barua - ujumbe ulioandikwa na ambao hutumwa kwa anayelengwa kupokea kwa njia ya posta

(iii) Simu - kifaa kinachotumiwa kuwezesha mawasiliano ya hewani kati ya watu

wawili walio mbalimbali

(iv) vidude - vifaa vinavyowekwa masikioni ili kunasa sauti kutoka kwa kifaa cha kidijitali ili kumwezesha msikilizaji kusikiza bila kutatizwa na watu wengine walio karibu naye.

(v) Stempu - kijikaratasi maalum chenye thamani fulani kinachobandikwa kwenye bahasha
kuidhinisha usafirishaji wa barua.
(vi) skrini - kiwambo cha simu ,mulishi .
(vii) mawasiliano - kupashana habari kati ya watu wawili au zaidi .

(f) Sentensi zijumuishe msamiati ulio katika (e). Sentensi pia zizingatie kanuni za sarufi .

2. Kite anaamka asubuhi ili kuelekea posta kutuma barua kwa ndugu yake anayeishi mjini. Anapanda gari na kukutana na Boke aliyekuwa akizungumza na mtu fulani kwa njia ya skrini.
Jambo hili linamshangaza .Boke anamshawishi Kite kuanza kutumia simu huku akimweleza kuwa simu si ghali kama alivyodhania . Kuwa simu hulingana na mfuko na uwezo wa mtu.
Boke anamshawishi Kite kununua simu na kukatiza safari yake ya kwenda posta

kutuma barua .

(b) Wasilisha muhtasari wako kwa wenzako wautolee maoni .

Dijitika (a- f)

Tekeleza shughuli hii kikamilifu .

Nje ya darasa(1-2)

Tekeleza shughuli hii kikamilifu

Shughuli ya 10: Kusoma kwa kina : Wahusika

1. (a) Ufisadi
(b) Uzembe/kukosa uzalendo/kutowajibika
(c) Kuwa msiri
(d) Kuwa mwenye ghadhabu /hasira

2. (a) Uwezo wa kufanya maamuzi mema hasa katika hali ngumu.
(b) Mpole - kutotumia lugha ya ukali / kutokasirika haraka.
(c) Kufanya kazi kwa bidii.

(d) Kuamini uwezo wa Mungu kufanya yote/ kusali mara kwa mara.
(e) Kuamini uchawi

(f) Kuuliza maswali mengi kuhusu asiyoyajua.

3. (a) wizi / udanganyifu haufai.
(b) Wema hauozi / mema unayofanyia wengine hukurudia .

(c) Mvumilivu hula mbivu / ni vizuri kutokufa moyo hata wakati mambo hayaendi vizuri kwani mwishowe kuna matumaini.
(d) Mpanda ngazi hushuka / si vyema kunyanyasa raia kwani mamlaka si ya milele/Unapotumia mamlaka vibaya,mwishowe utayapoteza na kuchukuliwa hatua za kisheria .
4.Vigezo vifuatavyo husaidia kutambua sifa za wahusika:
(i) Mandhari ya wahusika - Kwa mfano ikiwa mhusika anaishi katika mazingira yenye uchafu jambo hili linaweza kuonyesha yeye ni mzembe.

(ii) Matendo ya wahusika -Kwa mfano , mhusika anayepokea hongo ni fisadi .

(iii) Maneno ya wahusika wengine kuhusu mhusika fulani-Kwa mfano,mhusika

akimshukuru mwenzake kwa wema aliomtendea,atakuwa na sifa ya utu/ukarimu.

(iv) Maneno na maelezo ya mwandishi kumhusu –Kwa mfano mwandishi akidai mhusika

alitekeleza majukumu yake ipasavyo,atakuwa mwajibikaji.

(v) Maneno ya mhusika kujihusu yeye mwenyewe-kwa mfano akijisifu kuhusu jambo fulani,atakuwa mwenye majigambo/majisifu/majitapo.
(vi) Mambo anayopitia mhusika katika hadithi-Kwa mfano akipitia hali ngumu bila kukata tamaa,atakuwa mvumilivu.

5.(a) Tambua wahusika wote kwenye novela .Taja ni wepi wakuu , wadogo n.k
(b) Jadili sifa za wahusika kwa kuzingatia vigezo vya kutambua sifa za wahusika .

(c) Eleza mahusiano mbalimbali kati ya wahusika. Uhusiano huu unaweza kuwa wa kijamii , kikazi , kisiasa n.k
(d) Eleza kwa muhtasari sifa za kila mhusika uliyemtambua.
(e) Ili kutoa mafunzo zingatia mambo yanayowapata wahusika kwa kutekeleza

matendo fulani .

(f) Ukiwa na mwenzako igiza wahusika .

Dijitika

Ukitumia vifaa mwafaka vya kidijitali tekeleza shughuli a- c

Nje ya darasa

Shughuli a- c itekelezwe kikamilifu .

Shughuli ya 11 :Kusoma kwa mapana : Matini ya Kujichagulia

(a)Ujumbe wa matini haya ni kuwa watoto wana majukumu mengi katika viwango tofauti.Kuna majukumu ambayo yanawahusu wao wenyewe kama watoto binafsi . Kuna yale yanahusu marika yao , wazazi na walezi wao . Aidha watoto wana majukumu shuleni na kwa jamii kubwa kwa jumla .Wanapoyatekeleza,yatawapa nidhamu na kuwafanya kukubalika katika jamii.

(b) Matini haya yametumia msamiati ufuatao:

(i) majukumu

(ii) mawaidha

(iii) kibali

(iv) kijakazi

(v) wajibu

(vi) walezi .

(c) Rekodi msamiati ulioutambua .

(d) Rejelea kamusi ya Kiswahili sanifu kupata maana ya msamiati.

(e) (i) wajibu – jambo ambalo ni sharti litekelezwe na mtu fulani(jukumu)
(ii) faida - manufaa
(iii) kutii - kufuata maagizo
(iv) kijakazi - mfanyikazi wa nyumbani wa kike
(v) walezi - watu ambao si wazazi wa mtoto fulani ingawa wanamtunza na kumlea .
(vi) kuheshimu - kuwekea mtu adabu
(f) Sentensi zijumuishe msamiati uliopo katika (e)

(g) (i) amepiga mswaki - amesafisha meno kwa mswaki wenye dawa ya meno na maji

(ii) kupiga deki - kusafisha sakafu kwa kupitisha kitambaa chenye majimaji ili kuondoa uchafu

(iii) kutia bidii – kujikaza/kutia juhudi

(h) Muhtasari uandikwe kwa aya iliyounganisha hoja zifuatazo:

(i) Mtoto ni mtu aliye na umri mdogo.

(ii) Mtoto anaweza kuwa wa kuzaliwa na watu fulani au wa kupangwa na walezi fulani.

(iii) (iii) Watoto wana majukumu mengi katika viwango tofauti.

(iv) Wana majukumu yanayowahusu wao wenyewe , wazazi na walezi wao , shule , familia na jamii pana kwa jumla .

(v) Katika kiwango cha mtoto binafsi mtoto anafaa kuzingatia usafi wake.

(vi) Katika kiwango cha familia mtoto ana jukumu la kuwaheshimu wazazi au walezi wake , kusaidia na kazi za nyumbani na kulinda urithi na mali ya familia .

(vii) Watoto wana jukumu la kutangamana na marika yao kwa heshima na upendo .

(viii) Shuleni watoto wana jukumu la kutia bidii , kufuata kanuni za shule na kushiriki katika uongozi .

(ix) Katika kiwango cha jamii pana mtoto ana jukumu la kusaidia watu wenye mahitaji maalumu.

(i) Wasilishia wenzako muhtasari wako wautolee maoni .

Dijitika

Shughuli za a - f zitekelezwe kikamilifu .

Nje ya darasa

Shughuli za a na b zimikamilishwe nyumbani .

Shughuli ya 12 Kusoma kwa ufasaha

1.(a) (i) Matamshi bora ya sauti na maneno

(ii) Kusoma kwa kasi inayofaa

(iii) Kusoma kwa sauti inayosikika

(iv) Kutumia ishara zinazofaa

(v) Kusoma kwa kuzingatia toni na kiimbo kinachofaa

(b) Sakura mtandaoni kupata video inayorejelewa .

(c) Tathmini ni kiasi gani usomaji huo unazingatia vipengele vilivyoorodheshwa katika (a) hapo juu .

3. (a) Soma kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora .
(b)Shughuli itekelezwe.

Nje ya darasa

Tekeleza kikamilifu shughuli ya 1 na 2

Shughuli ya 13: Kusoma kwa kina : Mbinu za lugha uk 64- 66.

1 . Mbinu za lugha ni matumizi ya maneno au vifungu vya maneno ambavyo huipamba kazi ya fasihi na pia kusaidia kupitisha ujumbe .

2 (a) Mbinu za lugha ni matumizi ya msamiati na vifungu vyenye maana maalum katika maandishi ya kifasihi kwa namna yenye mvuto ili kupamba lugha na kupitisha ujumbe wa msanii kama alivyokusudia.

(b) Mwandishi ametumia mbinu za lugha kama vile :

(i) Tashbihi - kutulia sawia na maji mtunguni
- kuwa na sauti nzito kama simba

(ii) Nahau - ... akapiga moyo konde
(iii) Methali - mvumilivu hula mbivu - kikulacho ki nguoni mwako
(iv) Maswali ya balagha - Mbona Maria ananisaliti ? Au kikulacho ki nguoni mwako ?

(v) Sitiari - alikuwa kunguru
- Maria ni simba

(vi) Tashihisi/ uhaishaji - mawazo yalimteka nyara

- akachukuliwa na usingizi
(vii) Uzungumzi nafsia-Viola alijiuliza kimoyomoyo
(vii)Takriri-Hali hiyo ya sintofahamu...Hali ya kuhisi usaliti.Hali ya majonzi.Hali ya

kutamauka.Hali si hali.

(viii) Msemo-Usingizi wa mang'amung'amu

-roho kuwa mkononi

(ix)Taswira-Alijibanza katikati ya ukuta na ua na kutulia

(c) Zingatia mifano iliyotolewa katika (b) hapo juu .

(d) (i) Tashibihi - imetumiwa kulinganisha hali mbili . Kuonyesha jinsi ambavyo sauti ya Maria ilivyokuwa nzito ya kutisha kama ya simba,
Kuonyesha utulivu wa Viola kupita kiasi sawa na wa maji mtungini.

(ii) Nahau - imetumiwa kiufundi kuwasilisha maamuzi ya Viola ya kujipa moyo na ujasiri katika hali iliyomkabili.

(iii) Sitiari - tabia ya kunguru (woga) inahamishwa kwa Viola kusisitiza alivyoogopa, tabia ya simba (ukali) inahamishwa kwa Maria kudhihirisha ukali wake

(iv)Methali - imetumiwa kusisitiza umuhimu wa uvumilivu,
Ya pili yaonyesha jinsi ambavyo rafiki yake Viola ,Maria,alivyomsaliti licha ya uhusiano wao wa karibu

(v) Maswali balagha - maswali hayo yametumiwa kutuonyesha jinsi ambavyo Viola alivyokuwa amezongwa na mawazo yaliyodhihirisha kutoamini kwake kuwa rafikiye anaweza kumwendea kinyume.

(vi)Tashihisi - mbinu hii imetumiwa kuonyesha jinsi Viola alivyozongwa na mawazo nkulea mewa na usingizi .

(vii)Uzungumzi nafsia-Umetumiwa kuonyesha jinsi ambavyo Viola alikuwa na shaka kuhusu urafiki wake na Maria .

(viii)Takriri-Imetumika kusisistiza hali ya Viola ya sintofahamu na kutoamini kusalitiwa na rafikiye Maria.

(ix)Msemo-Wa kwanza waonyesha athari ya mawazo mengi aliyokuwa nayo Viola kiasi cha kuletea usingizi mzito,
Wa pili wasisitiza uoga mwingi aliokuwa nao Viola kutokana na hali iliyomkumba

(x)Taswira-Imetumika kutoa picha halisi ya jinsi ambavyo Viola alijificha bila kutaka kujulikana.

3.(a) Kawia ufike - Methali

(b)Yeye ni kasuku - Sitiari

(c) Si hayati si mamati - msemo

(d) Mrefu kama mlingoti - Tashbihi

(e) Baiskeli imeshika njia – Tashihisi/Uhaishaji

4. Zingatia mbinu za lugha zilizoorodheshwa katika **uk. 65** na majibu ya swali la **2b na 3 .**

Mifano mingine ya mbinu za lugha ni pamoja na:

(i) Taswira - Maelezo yanayojenga picha akilini mwa hadhira ya fasihi.

(ii) Kwelikinzani - Kauli zenye sehemu mbili zinazokinzana kwa mfano , Alicheka

kwa huzuni .

(iii) Kejeli – Maelezo yanayodhihaki hali fulani.

(v)Kinaya - Hali inayoenda kinyume na matarajio kwa mfano mtu mzembe kuzawadiwa kazini.

Tathmini ni zipi kati ya hizi mwandishi ametumia .

(b) Zingatia umuhimu wa mbinu mbalimbali ulioelezwa katika **uk 65** katika sehemu

ya kumbuka .

(c) Wasilisha kazi kwa mwenzako .

Dijitika

Shughuli a- c zitekelezwe kikamilifu .

Nje ya darasa

Shughuli a- c zitekelezwe kikamilifu .

Shughuli ya 14 : Ufahamu wa Kifungu cha mjadala

1 (a) Habari mahususi zilizozungumziwa katika kifungu hiki ni kuhusu njia mbalimbali za kupata natija , uekezaji , njia za kuweka akiba pamoja na nidhamu katika matumizi ya pesa kwa wanachama cha waendeshaji pikipiki.

(b) Ili awashauri wanachama kuhusiana na maswala yanayohusu kuchuma pesa , kuweka akiba na nidhamu katika matumizi yake.

(c) Msamiati mpya unaweza kujumuisha maneno yafuatayo :

(i) mapato

(ii)mtaji

(iii) akiba

(iv) wekeza

(v) mjasiriamali

(vi) mkopo

(d) hazina - mali au pesa zilizohifadhiwa kwa matumizi ya baadaye .

2 (b) Habari muhimu za kifungi hiki kwa ufupi zijumuishe hoja zifuatazo:

(i) Wanachama cha waendeshaji pikipiki walimwalika mtaalamu wa masuala ya fedha kwa kutaka kuelekezwa katika mambo mbalimbali.

(ii) Mshauri katika uelekezaji wake alichukua mkondo wa mjadala .

(iii) Wanachama walielekezwa kuhusu njia mbalimbali za kukuza mtaji na kuweka hazina .

(iv) Mshauri aliwaondolea hofu kuhusiana na kupotea kwa hazina yao kwa kuwaambia kuwa serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha usalama wa mtaji.

(v) Wanachama waliondoka kwenye kikao hicho wakiwa wamefaidi pakubwa kutokana na ushauri huo.

(c) Baadhi ya wanachama walionekana kupendelea njia za zamani za kuweka hazina kama vile kuweka pesa chini ya godoro wakidai kuwa njia za kisasa kama vile benki si salama jambo ambalo lilikinzana na maoni ya mshauri .

(d) Muhtasari ujumuishe hoja zilizoko katika jibu la **2 (b)** hapo juu.
Ziunganishwe kujenga aya .

Nje ya darasa

Shughuli za a- d zitekelezwe kikamilifu .

Shughuli ya 15: Ufupisho

1. (a)Aya ya 1: Maadili ni mwenendo na tabia njema ambayo mtu anatarajiwa kuwa nayo na jamii.

2. Aya ya 2: Mavazi ni sehemu ya maadili na mtu anafaa kuvaa mavazi yenye heshima kwani humtambulisha.

   Aya ya 3: Kila mtu anatarajiwa kuzingatia adabu njema anapoongea kwa kuyapima maneno yake.

   Aya ya 4: Twafaa kujiheshumu,kuwaheshimu watu wote kila wakati, mali yao pamoja na mali ya umma.

   Aya ya 5: Ni wajibu wa kila mtu kuwa na maadili,awe mwaminifu na mkweli popote pale ajipatapo.

   (b) Maadili ni mienendo mizuri ya mtu inayokubalika na jamii.Hudhihirika kupitia :mavazi yenye heshima yanayositiri sehemu zote za mwili,maneno yaliyopimwa kutoka kinywani mwa mja anapozungumza,heshima anayodumisha kwake,kwa wengine wote,kwa mali yao na kwa mali ya umma kila wakati. Kila mtu ana wajibu wa kuhakikisha kuwa anazingatia maadili yanayostahili popote pale.

   (c) Maadili ni tabia njema ambayo kila mtu anatarajiwa kuwa nayo katika jamii yake kwani hivyo atakubalika. Mtu anafaa kuvaa mavazi yenye heshima yanayositiri mwili wake vyema kwa kuwa mavazi humtambulisha. Aidha,anastahili kuzingatia utumiaji wa maneno yenye heshima anapozungumza na wenzake ili kuepuka kuwaudhi kwa kuropokwa.Heshima inafaa pia idumishwe kila wakati kwa wakubwa na wadogo bila ubaguzi .Huonekana jinsi mtu anavyokaa mbele ya watu,anavyowaamkua wakubwa wake na kuwahudumia watu bila ubaguzi. Ni sharti mja ajiheshimu,awaheshimu wenzake,mali yao pamoja na mali ya umma.Kila mtu anawajibu wa kuhakikisha kuwa anazingatia maadili na kuwa mwaminifu na mkweli popote ajipatapo.

   (maneno 101)

   (d) Rejelea hatua zilizoorodheshwa katika sehemu ya **kumbuka uk 70**.

3. Shughuli ya a na b zikamilishwe .

Nje ya darasa

Shughuli ya 1 na 2 zikamilishwe

3. Kuandika

Majibu

Shughuli ya 1: Viakifishi: Herufi kubwa na kikomo

I. Herufi kubwa

1. (a) Herufi kubwa: M, T, UKIMWI, N, M, L, M, H.
   (b) Kuanza sentensi, kuonyesha akronimu, kuonyesha nomino ya pekee, kuonyesha mwanzo wa nukuu.
   (c) Soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 71.

2. (a)Ameoga
   (b) Uganda
   (c) Kifaransa
   (d)Lo!
   (e) Bw. Kizito
3. (a) Mimi hupiga mswaki kila asubuhi.
   (b) Kibet na Salome walizuru mbuga ya wanyama.
   (c) Alituma barua kwa S.L.P 333, Meru.
   (d) Mteja aliuliza, "Utakuja lini tena?"
   (e) Mwandishi aliandika kitabu chenye mada 'Jana si leo'.

II Kikomo

1. (a) (i) Mwishoni mwa kila sentensi
   (ii) katika ufupisho wa neno Dkt.
   (iii) katika tarakimu 0.5
   (iv)katika tarakimu 100, 055.70.
   (b) Kuonyesha mwisho wa sentensi, kuonyesha neno lililofupishwa na kuonyesha tarakimu za nukta.
   (c) soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 73.

2. (a) Atasafisha.
   (b) Bi. Musembi
   (c) 0.3
   (d) La.
   (e) Shilingi 300.50.
3. (a) Nitafua nguo zangu leo.
   (b) Alishangaa alipotumiwa shilingi 5.50 kwa njia ya simu.
   (c) Mwanafunzi alifunzwa na Bw.Muhati.
   (d) 0.25 ni sawa na robo.
   (e) Barua ingefika asingekosea S.L.P.

Shughuli jumuishi

Ekwee alifaa kusafiri siku hiyo ya Ijumaa kuelekea Afrika Kusini. Aliamka asubuhi na kujinadhifisha kwa kuoga na kupiga mswaki. Baada ya kujipaka mafuta na kuvaa nguo safi,alichukua pasipoti yake na stakabadhi za usafiri zilizoandikwa 'Bw.Ekwee', ambazo alikuwa amezipata kwa shilingi 75, 347.70, akapanda teksi na kuelekea

uwanja wa ndege. Huko, alitangamana na watu waliozungumza Kiswahili, Kingereza na Kifaransa. Akiwa angani, aliona Mlima Kilimanjaro na Mto Limpopo. Kule Afrika Kusini, angepokelewa na rafiki yake Dkt. Njeri na pamoja wangesherehekea Siku kuu ya Pasaka.

Shughuli ya 2: Barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko

1. Kwa majibu ya swali hili, soma kiangaza katika uk wa 74 na sehemu ya 'kumbuka' katika ukurasa huo.
2. Tafiti ili kujibu swali hili.
3. (a) Mwaliko kwa sherehe ya siku ya kuzaliwa.
   (b) Kutaka kujua hali masomoni, fahamisho kuhusu siku ya kuzaliwa, mwaliko kwa sherehe ya siku hiyo, fahamisho kuhusu mahali sherehe itafanyika na watakaohudhuria, mada kuu ya mgeni mwalikwa,tumbuizo la siku pamoja na vyakula vitakavyoandaliwa.
   (c) Kwa jibu la swali hili, soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 76.
   (d)Shughuli hii itekelezwe.
   (e) Kwa jibu la swali hili, soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 77.
   4.(a) na (b) Tekeleza shughuli hizi.

Shughuli ya 3: Insha za kubuni

1. Kwa jibu la swali hili soma kiangaza katika uk wa 77.
2. (a), (b), (f), (g).
3. Vigezo:
   -chagua mada unayoielewa,
   -kisa kiwe cha kusisimua,
   -tumia lugha ya kuvutia,
   -kuwe na mzozo na utatuzi wake.
4. Tafiti ili kujibu swali hili.
5. (a) Vidokezo
   - Nani hakusikia au kufuata ushauri?
   - Alifanya nini?
   - Nini kilimfika?
   - Tunapata funzo gani kutoka kwa kisa chake?
6. Vidokezo vitokane na mada 'Mpanda ngazi hushuka'.
   Kwa mfano,
   -Ni nani alipata maendeleo/madaraka gani?
   -Hali yake mpya ilimuathiri vipi?
   -Ni vipi alirudi chini?
   -Funzo lipi linapatikana katika kisa hicho?

Shughuli ya 4: Insha za kubuni: Masimulizi

1. Elekezwa na sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 80 – 81.
2. (a) Nahau – akatia breki,
   Tashbihi – yalinguruma kama radi,tulitembea polepole kama kobe,
   Tashhisi – basi lilichapuza, ndege waliimba na kutushanglia,
   Taswira – msitu ulikuwa na miti mizuri,niliweza kuona maporomoko ya maji

Tabaini-si watoto,si wanawake,si wanaume,si watalii,
Msemo-kila mtu alikuwa katika hamsini zake
Tanakali za sauti-maji yalionekana meupe pepepe!
Methali-polepole ya kobe,humfikisha mbali

(b) Kuongeza ladha katika habari, kuleta picha halisi ya hali ilivyokuwa, kuleta uhalisia wa mazingira,
(c) Wahusika: Susana(msimulizi), mwenyeji wake Gilbert, watoto, wanawake, wanaume, watalii,ndege na tumbili
(d) Umuhimu wa mhusika ni nafasi aliyoichukua katika hadithi.Jadiliana na mwenzako.
(e) Mandhari: barabarani, msituni, pangoni, mbugani,mjini
(f) Mandhari hayo yamewezesha matukio tofauti kufanyika katika hadithi, kwa mfano barabarani kusafiri, mbugani kuona wanyama,mjini kupata chamcha,n.k

Shughuli ya 5: Insha ya maelekezo

1. (a) Soma kiangaza katika uk wa 83.
   (b) Ni insha ya maelekezo kwa kuwa inamwongoza mwanafunzi kwa njia bora ya kuandika insha bora katika mtihani wake kwa kuzingatia vigezo vyote muhimu hivyo kumweka katika nafasi ya kupata alama bora zaidi.
   (c) Sifa za insha ya maelekezo:
   kuwepo kwa mada, maagizo yafuatane kimtiririko, maelezo ya kutelekeza jambo yagonge ndipo, lugha sahili itumiwe, lugha ya kimafumbo iepukwe,maagizo yatoke upande mmoja, habari sahihi pekee itolewe.

2 na 3 Shughuli zitekelezwe

Shughuli ya 6: Insha za masimulizi: Picha

1. (a) Ni insha ya masimulizi- kisa kinaelezwa, matukio yanatiririshwa, wakati uliopita umetumiwa.
   (b) Mvua ya masika
   Hakuna masika, yasiyokuwa na mbu
   (c) Magari yamesombwa na maji, nyumba zimezama majini, miti imeng'olewa.
   (d) Msimu wa masika ulichelewa, ulipofika mvua ilinyesha kupindukia na kusababisha hasara kubwa, watu wengi waliathirika, shule hazikufunguliwa kwa muda, mvua ilipoisha mimea mingi ilichipuka na kuwafaidi binadamu na wanyama, msimulizi alikuwa kwa nyanyake msimu huo wote na kumfaa.

2. Andika insha, zingatia vipengele katika sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 87.
3. Fanya utafiti ili kujibu.

Shughuli ya 7: Insha za kubuni: Maelezo

1. Lugha rahisi pamoja na msamiati ufaao ili maelezo yaeleweke moja kwa moja.
2. (a) Kwa jibu, soma kiangaza katika uk wa 88.
   (b) Msamiati wote uliotumiwa ili kutoa maelezo, pamoja na semi, methali, nahau na uradidi.

(c) Kufanya ujumbe ueleweke zaidi.

3. Rejelea mfano wa insha uliyopewa ili kufanya zoezi hili.
4. Rejelea mfano wa insha uliyoisoma ili kufanya zoezi hili.

Shughuli ya 8: Kuandika viakifishi: Kiulizi na koma

I Kiulizi

1. (b), (c),na (g).
2. Kuuliza swali.
3. Andika kifungu, fuata maagizo.
4. Andika sentensi zozote mbili ambazo ni maswali, ziwe na kiulizi mwishoni.

II Koma

1. (a), (b), (c), (d), (e),na (f).
2. Kuonyesha pale msomaji anafaa kutua na pia kutenga tarakimu.
3. (a) Tazama jedwali hapa chini.
   (b) Tunga sentensi, tumia koma ifaavyo.
4.

Matumizi	Mfano
(a) Kutenga tarakimu	9, 887, 279
(b) Kuonyesha mtajo	Kwa mwalimu mkuu,
(c) Kutoa maelezo ya ziada	Mkulima, ambaye alipata hasara, amehama.
(d) Kabla ya usemi halisi	Mama alisema, “Nitaenda sokoni leo.”
(e) Kuandika anwani	S.L.P 3040, Tanga.
(f) Kutenga vitu vilivyo katika orodha	Nilinunua sukari, mkate na chumvi.

5. Tekeleza shughuli hii
6. (i) Nakwambia,leo utakuwaa nami mbinguni.
   (ii) Nakwambia leo, utakuwa nami mbinguni.
7. Rejelea jedwali katika 4. hapo juu

Shughuli jumuishi

(a) Je, wajua kwamba ulanguzi wa binadamu ni tatizo sugu, si tu katika eneo hili ,lakini pia katika ulimwengu mzima? Waziri Mkuu Bwana Ali Hamisi, jana aliorodhesha hatua nne kuu ambazo mataifa ya eneo hili yanazingatia ili kutatua tatizo hili. “Serikali yetu ikishirikiana na mataifa mengine itatekeleza hatua hizo,” alisema Waziri Mkuu. Na je ,hatua hizo zenyewe ni zipi? Hatua hizi ni pamoja na kupanua uwezo wa vyombo vya dola, kukabiliana na walanguzi, kubadilisha sheria ili kutoa adhabu kali kwa walanguzi na kuhimiza ushirikiano na makundi yasiyo ya kiserikali.

Shughuli ya 9: Insha za kubuni: Masimulizi

1. Kwa jibu la swali hili, soma sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 92.

2. Elekezwa na sehemu ya ‘kumbuka’ kutambua vipengele vya kujenga wazo katika insha hiyo.
3. Andika insha, fuata mfano uliopewa.
   Tekeleza shughuli ulizoagizwa.

Shughuli ya 10: Barua ya kuomba msamaha

1. (a) Kuonyesha kujutia kosa, kuomba msamaha.
   (b) Kuchelewa shuleni au kazini, kukosa nidhamu, kupoteza kitabu cha shule, kutovaa sare rasmi, kutohudhuria shughuli fulani.
   (c) na (d), soma kielelezo cha barua katika uk wa 95 – 96.

2. (a) Lugha ya upole, lugha nyenyekevu, lugha ya kuonyesha majuto, kutoa ahadi .
   (b) Ili kueleza sababu za kuchelewa kurudi shuleni na kuomba msamaha kwa jambo hilo.
   (c) Ameeleza sababu za kuchelewa, akaeleza mipango yake ya kufidia muda aliokosa shuleni atakaporejea na atakavyolipa karo.
   (d) Anwani ya mwandishi, anwani ya mwandikiwa,mtajo, sababu ya kuandika barua, kuomba msamaha, kutoa ahadi.
   (e) Atumiwe mada za masomo pamoja na mazoezi ili kufidia muda uliopotea.

3. Andika barua, fuata mfano uliopewa.

Shughuli ya 11: Insha ya maelezo

1. (a) Tazama sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 88.
   (a)na (c) kwa majibu, soma sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 98.
   2. (a) Mada – Haki za watoto, utangulizi – ufafanuzi, mwili – maelezo kuhusu haki za watoto na hitimisho – kauli ya mwandishi.
   (b)Vidokezo: haki ni nini,watoto ni kina nani, haki zao ni zipi,umuhimu wa watoto kupewa haki zao,jukumu la wazazi na walezi kwa watoto na kauli ya mwisho/mwito.

Shughuli ya 12: Hotuba ya kupasha habari

1. Kwa jibu la swali hili, soma kiangaza katika uk wa 99.
2. (a) Kielelezo A.

(b) Kuwakumbusha kwamba shule iko katika mazingira yaliyohatarisha usalama wake.Hata hivyo, msimamizi wa usalama shuleni yuko imara kwa kuwa hali hiyo ya siku iliyotangulia jioni ilidhibitiwa na jamii ya shule iwe na uhakika wa usalama wake.

(c)Shule kupakana na mtaa wa mabanda wa Njugu ambao huhofiwa kuwa tishio kwa usalama wa jamii ya shule.

3. (a)Muktadha ambamo kuna ongezeko la maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI hasa miongoni mwa vijana.
   (b) Namna virusi vya ukimwi husambaa na jinsi ya kujiepusha nao.
   (c) Nyepesi, msamiati wa kawaida, yenye adabu.
   (d) Soma sehemu ya ‘kumbuka’ katika uk wa 101.

4. (a) Vidokezo:

-kutambua magonjwa yanayoambukiza
-dalili zake
-athari zake
-njia za kuyatibu
-njia za kujikinga kutokana nayo
(b)Andika hotuba, fuata mfano uliopewa.
(c)Shughuli itekelezwe.

Shughuli ya 13: Insha za kubuni: Maelezo

1. (a) Soma kiangaza katika uk wa 102.
   (b) Soma sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 103.

2na3. Andika insha ukifuata maelekezo na mfano uliopewa.

Shughuli ya 14: Insha ya maelekezo

1. (b) (d), (e),na (f).
2. (a), (b), (d), (f), na(h).

3, 4 na 5. Fanya mazoezi haya kwa kurejelea mifano ya awali na pia mfano katika uk wa 105.

6. (a) Maelekezo

(b) Mada, lugha nyepesi, maelezo kutoka upande mmoja, maelezo ya hatua kwa hatua, marejeleo ya sehemu maarufu njiani.

(c) Mpangilio wa hatua za kuelekeza ni wa mtiririko kuanzia mwanzo wa safari hadi mwisho.Barabara,majengo na magari maalum pamoja na muda wa usafiri umeelezwa kwa njia inayoeleweka kwa urahisi,hatua kwa hatua kumwelekeza msafiri kufika anakoelakea.

7. Fanya zoezi hili, fuata mfano na maelekezo uliyopewa katika uk wa 105.

Shughuli ya 15: Kuandika kidijitali: Baruapepe

1. (a) Mtajo: Kwa maswahiba wangu, kuwajulia hali, shukurani kwa msaada, kuwaalika tena.
   (b) Anwani ya mwandishi, salamu, kuwajulia hali, kurejelea waliyoyafanya pamoja, mwaliko,mapambo ya lugha.

2. Fanya zoezi hili, rejelea zoezi la 1 na sehemu ya 'kumbuka' katika uk wa 107.

4. Sarufi

Shughuli ya 1

I. Nomino za pekee

1. Majina halisi ya watu (Bi. Kilinda, Kerubo),majina ya mito (Mto Njoro,Mto Tana), majina ya mahali(Mandera,Turkana), majina ya maziwa(Ziwa Nakuru,Ziwa Elementaita)Anwani ya vitabu(Zawadi ya Thamani,Kiu)n.k
(taja vitu vinavyoonekana katika mazingira yako)
2. Ayubu, Narok, Sudani, Ijumaa, Juni, Kikamba, Mto Athi, Afrika, Zebaki
3. (a) (i) Chozi la Heri
(ii) Nanyuki
(iii)Ali , Kurani
(iv) Somalia, Afrika
(v) Januari
(b) (i) anwani ya kitabu
(ii) mahali
(iii) jina halisi la mtu,kitabu kitakatifu
(iv) jina la nchi, jina la bara
(v) mwezi
4. majina ya watu, mahali, nchi, siku za wiki, miezi, vitabu vitakatifu, majina ya lugha, mito, maziwa, bahari, mabara, milima, sayari, vitabu (rejelea uk 108-109)
5. (a) Kigali - mahali
(b) Jumatano – siku ya wiki
(c) Biblia – kitabu kitakatifu
(d) Mshtarii, Zohali – sayari
(e) Mokeira – jina la mtu, Kikisii, Kiswahili, Kingereza – lugha
6. Adele, Veronica, Tusomeni JS, Mto Kiberenge,
7. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo:
(a) Nitafua nguo zangu zote siku ya Jumapili.
(b) Marashi aliyojirashia yalinunuliwa Marekani.
(c) Sayari ya tatu kutoka kwa jua ni Dunia.
(d) Blanketi zangu zitaoshwa likizo ya Aprili.
(e) Vugutsa anachana nywele zake.
8. Zingatia sarufi na uakifishaji hasa wa nomino za pekee(zianze kwa herufi kubwa).
Kifungu lazima kihusu usafi wa kibinafsi.

II. Nomino za kawaida

1. kitabu, dawati, kalamu, karatasi, chaki, ubao, darasa, mlango, ukuta, sakafu, dirisha, mwalimu, mwanafunzi, msichana (Mifano hii imezingatia mazingira ya darasani. Taja kulingana na mazingira ulimo.)
2. kitabu, mti, kiti, saa, karatasi, simu, kalamu, pasi
3. (a) (i) riwaya, wiki
(ii) nauli, ndege
(iii) maji, mto, vibuyu
(iv) wapishi, matunda

(v) wanafunzi
(b) (i) vitu
(ii) vitu
(iii) vitu
(iv) watu, vitu
(v) watu
4. chupa, penseli, tarakilishi, maua, miti, shule, sofa, rangi, picha, taa, runinga, kitanda, blanketi (hii ni baadhi ya mifano)
5. (a) chupa, meza – vitu
(b) sabuni – kitu
(c) kiongozi – mtu, kura, kazi –vitu
(d) mtoto – mtu, barabara, kivukomilia – vitu
(e) lugha, hadhi – vitu
6. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano ya sentensi ni kama ifuatayo.
(a) Dora alipangusa uchafu uliokuwa kwenye sofa.
(b) Nguo safi zilikunjwa na kuwekwa kwenye boksi.
(c) Njia ya kuingia numbani ilifagiliwa.
(d) Wakulima huosha chuchu za ng'ombe kabla ya kuwakama.
(e) Riziki alipiga deki nyumba kasha akaenda bafuni kuoga.
7. Zingatia sarufi na uakifishaji hasa mwanzoni mwa sentensi. Kifungu lazima kihusu usafi wa kibinafsi.

Dijitika
1. Andika kifungu ulichopewa kwenye kifaa cha kidijitali.
2. **Jumatatu** ya wiki ijayo itakuwa siku ya **Krismasi**. Shangazi yangu **Rebeka** amenialika pamoja na ndugu zangu tuende kwake **Eldoret** kusherehekea naye. Ameahidi kutupikia vyakula vya aina nyingi ikiwemo mahamri. Binamu zetu, akina **Veni**, pia watakuwa. Ametuahidi kuwa baada ya sherehe, atatuwekea filamu maarufu ya **Vijana wa Leo** ambayo imezinduliwa juzi. Ila ametupa sharti moja kuu: Lazima tumsaidie kuosha vyombo na kunadhifisha nyumba kabla ya kutazama filamu hiyo.

Nje ya darasa
1. Onyango, Biblia, Mto Yala, Ziwa Viktoria, Kijaluo (zingatia mazingira yenu ya nyumbani)
2. sahani, kikombe, vijiko, jiko, sufuria, kiti, chakula, nyumba, mimea, jembe, redio, paka (taja nomino za kawaida nyingi iwezekanavyo)

Shughuli ya 2:
I. Nomino za makundi
1. (a) shungi
(b) kikosi
(c) bumba
(d) mkungu wa ndizi
(e) baraza la wazee
2. (a) mlolongo wa magari, umati wa watu, msitu wa miti

(b) darasa la wanafunzi
3. (a) shungi la nywele
(b) kicha cha funguo
(c) halaiki, msafara
(d) bunda la noti, shada la maua
(e) thurea ya nyota
4. dazeni ya mayai, umati wa watu, shungi la nywele, jozi ya viatu, binda la noti, mlolongo wa magari, msafara
5. (a) mazingira ya shuleni – darasa la wanafunzi, dazeni ya penseli, timu ya kandanda, kikundi cha wanafunzi (Hii ni mifano tu)
mazingira ya nyumbani – dazeni ya mayai, tone la maji, seti ya sofa, jozi ya viatu, doti ya kanga (Hii ni mifano tu)
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano:
*Mwalimu alinunua **dazeni ya penseli** kutoka dukani.*
***Timu ya kandanda** ilicheza vizuri.*
*Sebuleni mwetu mna **seti ya sofa**.*
Mama alipanga) ***doti ya kanga** sandukuni mwake.*
6. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) **Kikosi cha askari** kilishambulia majambazi.
(b) Mgeni mwalikwa alikaribishwa na **darasa la wanafunzi**.
(c)Bi harusi alivishwa shada la maua.
(d) Muuzaji alifungua **robota la nguo** nzuri sokoni.
(e) **Umati wa watu** ulifumukana mkutano ulipoisha.
7. (a) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Sentensi zihusu lishe bora. Mfano: Wanyonyi alimega **tonge la ugali** akala kwa mchicha.
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika kifungu. Kifungu kihusu lishe bora.

II. Nomino dhahania
1. (a) shibe
(b) ukarimu
(c) huzuni
(d) kiu
(e) wema
2. (a) simanzi
(b) uzuri
(c)lishe, afya
(d) woga, ukali
(e) utamu, raha
(f) uchungu, usingizi
3. uzalendo, amani, upendo, uvivu, chuki, hasira, upole, utu, heshima, werevu, maadili, maarifa, uchoyo, ukatili, wivu, uvivu, tamaa, elimu
4. (a) Mazingira ya shuleni – furaha, werevu, uzuri, bidii, ushindi, huzuni, wema, uongozi(Hii ni mifano tu)

Mazingira ya nyumbani – unadhifu, lishe,huzuni,ushirikiano, upendo, upishi, ukarimu, utu(Hii ni mifano tu)
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano:
*Kila mtu alijawa na **huzuni** timu yetu iliposhindwa.*
***Uongozi** wa shule hii unafaa kumthamini kila mwanafunzi.*
***Unadhifu** wa sebule huwavutia wageni.*
*Tunafaa kuwarekebisha watoto kwa **upendo**.*
5. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) **Ujeuri** wao uliwatia matatani.
(b) Mwalimu alijawa na **furaha** wanafunzi walipokamilisha mradi.
(c) **Wema** wa Bwana Abenga ulimfanya atambulike kote.
(d) Dawa alizokunywa zilitibu **ugonjwa** wake.
(e) Wasichana wa jamii ile wana **urembo** usiomithilika.
6. (a) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Sentensi zihusu lishe bora. Mfano: ***Lishe** ya watoto hawa ilikuwa na virutubisho vyote.*
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika kifungu. Kifungu kihusu lishe bora.

Shughuli jumuishi
(a) Matone ya maji, msitu, mlolongo wa magari, halaiki ya watu, timu, umati
(b) baridi, Upepo, nguvu, huzuni, simanzi, umoja, uzito, maarifa, ushindi, raha

Dijitika
(a) Tafuta kifungu kuhusu lishe bora mtandaoni. Tambua kwanza nomino za makundi na nomino za dhahania kwenye kifungu uzitenganishe ukitumia jedwali kama hili.

Nomino za makundi	Nomino za dhahania

(c)Sambazia wenzako jedwali lako mtandaoni.

Nje ya darasa
1. Fanya zoezi hili kwa kushirikiana na mzazi au mlezi. Unaweza kuandika nomino ulizozitambua daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali.
2. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi kwa kila nomino uliyoitambua. Ziandike daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali. Msomee mzazi au mlezi sentensi zako.

Shughuli ya 3:
I. Nomino za wingi
1. (a) maziwa, mafuta
(b) asali
(c) sukari, asali, chai
(d) maji, maziwa
(e) marashi

(f) maziwa
(g) manukato
2. (a) Mifano: maji, usaha, maziwa,
(b) Sentensi ziwe sahihi kisarufi. Mifano ya sentensi:
*Mifugo wana haki ya kupewa lishe bora na **maji** ili wawe na afya bora.*
*Punda mwenye uvimbe wenye **usaha** alipewa matibabu.*
*Ng'ombe wake alipougua na kushindwa kutoa **maziwa**,alimleta daktari wa mifugo nyumbani kumtibu.*
3. (a) wino, maji, mafuta, maandishi, mazingira
(b) Sentensi ziwe sahihi kisarufi.
4. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) Nyama ya nguruwe huwa na **mafuta** mengi.
(b) **Manukato** kutoka Ufaransa hunukia vizuri.
(c) Chakula kitamu kiliwafanya wadondkwe na **mate**.
(d) Simba hupenda kujificha kwenye **mazingira** yenye nyasi.
(e) **Mandhari** ya msitu wa Karura yanapendeza.
(f) Kiwanda hiki hutengeneza **sukari**.
(g) Bahari huwa na **maji** mengi kuliko mito.
5. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika kisa. Kisa kihusu uhuru wa wanyama.

II. Nomino za vitenzi-jina
1. (a) (i) Kulima
(ii) Kutesa
(iii) Kuwatunza
(iv) Kusafisha
(v) Kufanya
(vi) Kutuzwa
(vii) Kufugwa
(viii) Kudidimia
(b) Tunga sentensi ambazo ni sahihi kisarufi. Zingatia sentensi katika 1 (a) kama mifano.
2. (a) kusoma, kuimba, kuandika, kucheza, kutembea (Hii ni mifano tu)
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano ya sentensi:
Kusoma kwake kulifurahisha mwalimu.
Umati ulishngilia kuimba kwake.
Kucheza kwake kuliwapa ushindi kwenye timu yao.
3. (a) Kula kwa mtoto huyu kuna shida.
(b) Kuimba kwake kuliwafurahisha wengi.
4. (a) (i) kulima
(ii) kuimba
(iii) kucheza
(iv) kusafiri
(v) kula
(vi) kufa
(b) Tunga sentensi ambazo ni sahihi kisarufi. Sentensi zihusu wanyama. Mifano:

(i) **Kulima** kwa wanyama huchukua muda mfupi.
(ii) **Kuimba** kwa waombolezaji kuliendelea hadi alfajiri.
(iii) Waziri aliwatuza kwa **kucheza** kwao.
(iv) **Kusafiri** huku kuna manufaa mengi.
(v) Daktari alinihoji kuhusu **kula** kwangu.
(vi) **Kufa** kwa wanyama hao kulileta hasara.
5.Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika kisa. Kisa kihusu uhuru wa wanyama.

Shughuli jumuishi
1. (a)

Nomino za wingi	Nomino za vitenzi jina
chai, mchanga, maji, maziwa, marashi, manukato, unga, uji, chumvi, mate	kulima, kucheza, kuabudu, kuimba, kuandika, kufuga

(b) Tunga sentensi zilizo sahihi kisarufi kwa kuzingatia nomino zilizo katika jedwali la 1(a).
2. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu uhuru wa wanyama.

Nje ya darasa
(a) Unaweza kuandika nomino ulizozitambua daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali.
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi kwa kila nomino uliyoitambua.
Ziandike daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali. Wasomee wenzako darasani sentensi zako.

Shughuli ya 4:
I. Wakati uliopo
1. unapikwa, ninapangusa, yanaoshwa, unanunua, inakatwa
2. (a) wanakunywa
(b) kinatengenezwa
(c) anafua, anazianika
(d) inapakwa
(e) yanachimbwa
(f) panasafishwa
3. anapika, anakata, anakiweka, anaweka, anainjika, anawasha, anakata, kinapoendelea, ninajua.
4. (a) Watalii wanatembelea mbuga ya wanyama.
(b) Kucheza kwake kunawafurahisha wengi.
(c) Wanachota maji kwenye mto huu.
(d) Mvua inanyesha na inaleta baridi kali.
(e) Tunakwea mlima.
5. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) Mpira unachezwa.
(b) Wakulima wanalima.
(c) Karatasi zinapepea.
(d) Matikiti yanakatwa.

(e) Nyumba ile inabomolewa.
6. (a) (i) anapanda
(ii) yanamtatiza
(iii) vinasomwa
(iv) unamwagika
(v) zinafumwa
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
(i) Simba anapanda mwamba.
(ii) Magonjwa yanamtatiza.
(iii) Vitabu vyote vinasomwa.
(iv) Unga unamwagika.
(v) Fulana zinafumwa na nyanya.
7. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu aina za maliasili ikizingatia wakati uliopo.

II. Wakati uliopita
1. alipiga, alilima, waliomba, tulisafisha, mlikariri, ulikwea, nilipanda, waliona
2. (a) ilirekebishwa
(b) aliyetunza, alisifiwa
(c) uliokotwa, ilivyofaa
(d) zilishonwa
(e) ulikuwa
3. aliamka, alienda, alishukuru, yaliyofanya, alikata, zilizotosha, zilizotosha, alizifunga, yaliyoweza, alibeba, alipofika, alipata, alikuwa, aliweka, alipomaliza, aliwaweka, aliwawekea, aliyochota, walishiba
4. (a) Dawati lilijaa vitabu.
(b) Ziwa Viktoria lilijaa kutokana na mafuriko.
(c) Mlango ulipobishwa aliufungua.
(d) Mlima ulikuwa na theluji.
(e) Mtaala wa Umilisi ulikuza talanta.
5. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) Kwake shambani kulilimwa.
(b) Baada ya ndege kupaa, Kwamboka alitazama chini kwa huzuni.
(c) Umati ulishangilia mwanariadha huyo aliposhinda mbio hizo.
(d) Idhaa zilitangaza mchuano huo mubashara.
(e) Uga huu ulikarabatiwa mwezi uliopita.
6. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu aina za maliasili na izingatie wakati uliopita.

III. Wakati ujao
1. (a) itaoshwa
(b) yataisha
(c) utadakwa
(d) vitashonwa

(e) litapita
2. (a) atajiunga
(b) utajaa, watakaofika
(c) itatengenezwa
(d) zitafuliwa, zitaanikwa
(e) yatakuwa
3. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) Watalii watazuru mbuga hii mwezi wa Aprili.
(b) Kisima kitachimbwa mwaka ujao katika eneo hilo kame.
(c) Maziwa yatauzwa na wakulima sokoni.
(d) Matangazo yatatangazwa na mwanahabari mashuhuri.
(e) Gari la shehena litapita mpakani.
4. atatufunza , tutakapoamua, tutatengenezea, tutakapogundua, tutaanza, tutatembelea, tutafurahi.
5. (a) Darasa litasafishwa Ijumaa.
(b) Mazingira yatapendeza.
(c) Mlima utakuwa na theluji.
(d) Bahari itachafuka.
(e) Ziwa hili litakuwa na samaki wengi.
6. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
(a) Hadija atazuru pwani mwezi wa Agosti.
(b) Mwanaskauti atakwea Mlima Kenya.
(c) Wagonjwa wataona baada ya kufanyiwa upasuaji.
(d) Nyote mtapata chakula cha kutosha.
(e) Tukifuzu sote tutafurahi.
7. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu aina za maliasili.Wakati ujao uzingatiwe.

Shughuli jumuishi
1. (a) Baadhi ya sentensi ni kama vile; *Mama alichota maji./Halima alimsaidia mama./Maji yalijaa kwenye kibuyu./Mama alimwaga maji kwenye kibuyu.*
(b) Baadhi ya sentensi ni kama vile; *Wanafunzi walizuru mbuga ya wanyama pori./Wanafunzi waliona wanyama pori wengi mbugani./Mwelekezi aliwaeleza wanafunzi kuhusu wanyama pori mbalimbali.*
2. Katika sentensi ulizozitunga katika 1 (a) na (b), badilisha kiambishi -li- kiwe -na-.
3. Katika sentensi ulizozitunga katika 1 (a) na (b), badilisha kiambishi -li- kiwe -ta-.

Dijitika
1. Sentensi hizo lazima zitumie kiambishi -na- cha wakati uliopo. Zingatia sarufi na uakifishaji.
2. Wasambazie wenzako sentensi ulizozitunga ili wafanye walivyoagizwa.

Nje ya darasa
1. Sakura mtandaoni au vitabuni kupata matini ulivyoagizwa.

2. Somea mzazi au mlezi matini hayo.
3. Unaweza kuiandika kwenye kifaa cha kidijitali au daftarini kisha umsomee tena.

Shughuli ya 5:
I. Wakati uliopo hali ya kuendelea
1. (a) anasoma
(b) anahutubia
(c) anasakata
(d) inanyesha
2. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
*Barabara i**na**sakafiwa.*
Mtoto analishwa.
3. zinaendelea, anaongoza, anafuatiwa, anafuatilia
4. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu unyanyasaji wa kijinsia.

II. Wakati uliopita hali ya kuendelea
1. (a) alikuwa akifunza
(b) walikuwa wakicheza
(c) alikuwa akilia
(d) yalikuwa yakiendelea
(e) walikuwa wakiiunda
2. alikuwa akiikagua, alikuwa akiwaelimisha, alikuwa akitembea,walimkaribisha wakipiga,
3. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
Nyumba ilikuwa ikijengwa mvua ilipoanza kunyesha.
Wanafunzi walikuwa wakisoma darasani umeme ulipopotea.
3.Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu unyanyasaji wa kijinsia.

III. Wakati ujao hali ya kuendelea
1. (a) atakuwa akilala (b) atakuwa akisoma (c) atakuwa akiadhini (d) atakuwa akifua, atakapokuwa akipiga (e) utakuwa ukifika, tutakapokuwa tukianza
2. watakuwa wakishangilia, atakapokuwa akiingia, watakula wakishauriana
3. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
Sanamu itakuwa ikichongwa dukani.
Wachezaji watakuwa wakifanya mazoezi uwanjani jioni.
3.Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu unyanyasaji wa kijinsia.

Shughuli jumuishi
1. (a) Unyanyasaji wa kijinsia ulikuwa ukiendelea katika jamii. Viongozi walikuwa wakiomba wananchi washirikiane nao kuukomesha unyanyasaji huo. Kila mmoja alikuwa akijitolea kuhakikisha kuwa dhuluma hizi zilikuwa zikifikia kikomo.
(b) Unyanyasaji wa kijinsia utakuwa ukiendelea katika jamii. Viongozi watakuwa wakiomba wananchi washirikiane nao kuukomesha unyanyasaji huo. Kila mmoja atakuwa akijitolea kuhakikisha kuwa dhuluma hizi zitakuwa zikifikia kikomo.
2. (a) Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:

Muhula ulikuwa umeanza.
Wazee walikuwa wakishauriana barazani kuhusu usalama wa kijiji.
(b) Tumia kiambishi -na- cha wakati uliopo hali ya kuendelea. Mfano:
Muhula unaanza.
Wazee wanashauriana barazani kuhusu usalama wa kijiji.
(c) Tumia viambishi -ta- na -ki- vya wakati ujao hali ya kuendelea. Mifano:
Muhula utakuwa ukianza.
Wazee watakuwa wakishauriana barazani kuhusu usalama wa kijiji.

Nje ya darasa
1. Tumia kiambishi -na- cha wakati uliopo hali ya kuendelea katika aya yako. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga aya.
2. Msomee mzazi au mlezi ulivyoelekezwa.
3. Tumia viambishi -ta- na -ki- vya wakati ujao hali ya kuendelea.
4. Msomee mzazi au mlezi tena ulivyoelekezwa ili akupe maoni yake.

Shughuli ya 6:
I. Vitenzi vikuu
1. (a) wanalinda
(b) jenga
(c) chaguliwa
(d) ukilala
(e) akihakikisha
(f) akicheka
(g) kuchelewa
(h) atembee, kunyesha
(i) wakikaguliwa
(j) kukamilisha
2. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
Nyumba imekuwa <u>ikiezekwa</u> paa.
Wanariadha wameanza <u>kujitayarisha</u> kwa mashindano hayo.

II. Vitenzi visaidizi
1. (a) wangali
(b) utakuja
(c) iliweza
(d) nilikuwa
(e) aliwahi
(f) itabidi
(g) nitakuwa
(h) mngali
(i) sikuweza
(j) atakuja
2. Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:

Nyumba imekuwa ikiezekwa paa.
Tungali tunasoma miaka minne baadaye.
3. Mifano ya sentensi:
(a) Migodi itakuwa ikichimbwa.
(b) Mashamba yangali yanalimwa.
(c) Unaweza kuinua gogo hili?
(d) Mamba anataka kumkamata simba.
(e) Wewe umewahi kupanda ndege?

Shughuli jumuishi
1. Vitenzi vikuu – ukidorora, kuanzisha, kushirikiana, kudumisha, kuhakikisha
Vitenzi visaidizi – ulikuwa, aliamua, alitutaka, kuweza, aliapa
3.Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi.

Dijitika
(a) Tafuta kifungu kuhusu usalama shuleni mtandaoni kisha ukisome.
(b) Tambua kwanza vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi kwenye kifungu. Unaweza kuviandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali.
(c) Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga aya ukitumia vitenzi ulivyovitambua. Ziandike daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali.
(d) Sambazia wenzako kifungu chako mtandaoni ili wakitolee maoni.

Nje ya darasa
1. Tunga sentensi ulivyoagizwa.
2. Msomee mzazi au mlezi sentensi zako ili azitolee maoni yake.

Shughuli ya 7:
Vitenzi vishirikishi
1. (a) li (b) ndio (c) tu (d) ni (e)kuwa (f) si (g) vi (h) ndimo
2. (a) mu, ndizo, ni, ndisi, ndio, kumekuwa, yumo, li, pa, wapo, yungali, sicho
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji unapotunga sentensi. Mifano ya sentensi:
Embe hili li kikapuni.
Sisi ndisi wakulima bora kijijini.
3. Mifano ya sentensi:
(a) Pahali hapo palikuwa pachafu.
(b) Pake pamo madukani.
(c) Gari li safi.
(d) Wanafunzi walikuwa uwanjani.
(e) Hivi ndivyo vyangu.
(f) Huyu si wa timu yetu.
(g) Kule ndiko kwa Amina.
(h) Sisi ndisi wanafunzi bora zaidi.
(i) Kinda yu kiotani.
(j) Hana ana duka zuri.

4. (a) tu/ndisi/tulikuwa/ni /si(b) ndiye /siye(c)tulikuwa/hatukuwa (d) yu/yumo/angali (e) ni/alikuwa/si/ndiye (f) yu/amekuwa/alikuwa/yumo/angali (g) ni/ku/ndiko/si (h) li/limo/limekuwa /lingali(i) wana
5. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi katika aya. Aya ihusu kuhudumia jamii shuleni.

Nje ya darasa
1. Unaweza kurejelea uk 126 kwa maelezo zaidi.
2. Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Sentensi zihusu shughuli katika mazingira ya nyumbani. Mfano: *Mama yu jikoni.*
3. Msomee mzazi au mlezi sentensi ulizozitunga.

Shughuli ya 8:
I. Ngeli ya A-WA
1. (a) kiroboto, kuku, ng'ombe, mtoto, rafiki
(b) Fanya zoezi (b) na (c) kwa wakati mmoja. Tunga sentensi huku ukipigia mstari viambishi vya upatanisho wa kisarufi. Mfano: *Kiroboto anarukaruka.*
Viroboto wanarukaruka.
(c) Fanya zoezi hili pamoja na zoezi la (b)
2. (a) (i) viwavi, kipepeo, panzi, buu, funza
(ii) kiboko, simba, nguruwe, mbuzi, mbwa
(iii) msichana, wanafunzi, mpishi, Gesare
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mfano: *Mbwa anabweka.*
(c) Pigia mstari viambishi vya upatanishokatika sentensi zote ulizozitunga. Mfano: *Mbwa anabweka. Mbwa wanabweka.*
(d) A-WA
3. (a) Mbuzi ameuzwa. Mbuzi wameuzwa.
(b) Nyoka ameuawa. Nyoka wameuawa.
4. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano
(a) Mlanguzi amekamatwa. – Walanguzi wamekamatwa.
(b) Kiroboto amefyonza damu. – Viroboto wamefyonza damu.
(c) Dagaa anaelea majini. – Dagaa wanaelea majini.
(d) Mende anatembea ukutani. – Mende wanatembea kutani.
(e) Mtoto amezaliwa. – Watoto wamezaliwa.
(f) Mwalimu alitufunza ngeli. – Walimu walitufunza ngeli.
5. (a) Kiroboto aliruka motoni.
(b) Ng'ombe wake aliuzwa leo jioni.
(c) Watoto wale walikuwa wamelanguliwa.

Ngeli ya U-I
1. (a) mti, mkoba
(b) Zingatia sarufi na uakifishaji wa sentensi. Mifano:
Mti umeanguka. – Miti imeanguka.
Mkoba ulinunuliwa. – Mikoba ilinunuliwa.

(c) Pigia mstari viambishi vya upatanisho katika sentensi zote ulizozitunga. Mifano: *Mti umepandwa. – Miti imepandwa.*
Mkoba ulinunuliwa. – Mikoba ilinunuliwa.
2. (a) (i) mdomo, mgongo, mfupa, moyo
(ii) mbono, mkahawa, mkalatusi, mfenesi
(b) Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mfano
Mgongo umeumia. – Migongo imeumia.
(c) Mfano: *Mgongo umeumia. – Migongo imeumia.*
(d) U-I
3. (a) Mti ulianguka. – Miti ilianguka.
(b) Mkono ulitibiwa. – Mikono ilitibiwa.
4. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Mtaro umesafishwa. – Mitaro imesafishwa.
(b) Mwezi umeisha. – Miezi imeisha.
(c) Mwili umechoka. – Miili imechoka.
(d) Mtoumefurika. – Mito imefurika.
5. (a) Mkono wa mwizi yule ulikatwa/ Mikono ya mwizi yule ilikatwa.
(b) Mti umeanguka/ Miti imeanguka.

Shughuli jumuishi
1.

Ngeli ya A-WA	Ngeli ya U-I
mwizi, mbuzi, samaki, mende	mkono, mkoba, mfereji, mti

2.

Ngeli ya A-WA	Ngeli ya U-I
Mifano: mwalimu, mpishi, mchezaji, mama,mwanafunzi	Mifano: mwiko, mlima, mti, muhula,mkoba

3. (a) A-WA
(b) A-WA
(c) U-I
(d) A-WA
(e) U-I
4. (a) fanya zoezi hili na la (b) kwa wakati mmoja.
(i) Samaki mkunje angali mbichi.
(ii) Simba akikosa nyama, hula nyasi.
(iii) Ng'ombe akivunjika malishoni, hujikokota hadi zizini.
(iv) Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
(c) A-WA
5. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
A-WA *Mkora aligunduliwa. - Wakora waligunduliwa.*
U-I *Mtego uliwanasa majangili. – Mitego iliwanasa majangili.*

Nje ya darasa
1. Taja nomino kama vile:

A-WA- baba, nyanya, babu
U-I- mgongo, mkia
2. Zingatia upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

Shughuli ya 9:
I. Ngeli ya KI-VI
1. kitabu, kiti, kioo, kijiko, chakula
2. kitabu, kioo, kiti, choo, kijidole
3. (a) kibofu
(b) kibole
(c) chakula
(d) kichanio
(e) kitoto(Rejelea mapendekezo kitabuni ,uk 130 kuhusu *kiwavi na *kipepeo)
4. (a) kiatu, kisigino
(b) vidole, visiki, kijia
(c) vitambaa, kiuno
(d) kijana, kisu
(e) kishaufu, kipua
5. (a) (i) Kiserema kilitumiawa kupalilia mimea.
(ii) Kisukari kile kitaliwa leo.
(iii) Kitambi chake kimeisha baada ya kufanya mazoezi.
(iv) Kijilima kile kina kijia kinachofika kwenye kilele.
(v) Kitenge hiki kitatumika kushona nguo ya Asha.
(b) (i) Viserema vilitumiawa kupalilia mimea.
(ii) Visukari vile vitaliwa leo.
(iii) Vitambi vyao vimeisha baada ya kufanya mazoezi.
(iv) Vijilima vile vina vijia vinavyofika kwenye vilele.
(v) Vitenge hivi vitatumika kushona nguo za Asha.
6. (a) Kitimaguru kilimsaidia mgonjwa yule.
(b) Kitabu kiliwekwa ndani ya kijidawati.
(c) Kitoweo na kitumbua kilitayarishwa jana.
(d) Kifaa cha kidijitali kimerahisisha jambo.
(e) Kipakatalishi kimenunuliwa.
7. (a) ki
(b) vi
(c) vi
(d) ki
(e) vi
8. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Kitunguu kimekatwa. Vitunguu vimekatwa.
(b) Choo kimeoshwa. Vyoo vimeoshwa.
(c) Kitasa kimeharibika. Vitasa vimeharibika.
(d) Kisanduku kimepakwa rangi. Visanduku vimepakwa rangi.
(e) Kiwiko kimeumia. Viwiko vimeumia.

9. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika aya yako.

II. Ngeli ya LI-YA

1. (a) gari, darasa, gwaride, ua,dirisha
(b) gari, jiwe, chungwa, jijumba, kombe
2. (a) chungwa
(b) beseni
(c) jisu
(d) ua
(e) madoa
3. tumbo, jungu, mafiga, kabati, parachichi, maembe, papai, beseni, embe, boga, jilango, jumba,jina
4. (a) (i) Majumba yalijengwa karibu na majijito yaliyokauka.
(ii) Mananasi yaliyochumwa yaliliwa.
(iii) Mabega yao yameumia.
(iv) Mashanuo haya huchana nywele vizuri.(*hakipo,napendekeza-Mashanuo haya yalichana nywele vizuri)uk 132
(v) Matawi makubwa yalikatwa.
(b) (i) Jumba lilijengwa karibu na jijito lililokauka.
(ii) Nanasi lililochumwa lililiwa.
(iii) Bega lake limeumia.
(iv) Shanuo hili huchana nywele vizuri.(*pendekezo-Shanuo hili lilichana nywele vizuri)
(v) Tawi kubwa lilikatwa.
5. (a) li
(b) ya
(c) ya
(d) li
(e) ya, ya
6. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Shina limekauka. Mashina yamekauka.
(b) Shati limeoshwa. Mashati yameoshwa.
(c) Jikombe limewekwa uji. Majikombe yamewekwa uji.
(d) Tufaha limenunuliwa. Matufaha yamenunuliwa.
(e) Sharafa limenyolewa. Masharafa yamenyolewa.
7. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika aya yako.

Shughuli jumuishi

1. (a) kikoi, kinanda, kijiti, kitoweo, kikombe
(b) Fanya zoezi la (b) na (c) kwa wakati mmoja. Mfano:
Kikoi chake kimezeeka. Vikoi vyao vimezeeka.
2. (a) jikoi, jinanda, jijiti, jitoweo, jikombe
(b) Fanya zoezi la (b) na (c) kwa wakati mmoja. Mfano:
Jikoi laake limezeeka. Majikoi yao yamezeeka.

3. Nomino zikiwa katika udogo huwa katika ngeli ya KI-VI na zikiwekwa katika ukubwa huwa katika ngeli ya LI-YA.

Nje ya darasa.
Mifano:
KI-VI- kiota, kitanda, kiti
LI-YA- shamba, tunda, gari, rinda

Shughuli ya 10:
I. Vinyume vya maneno
1. Rejelea uk 133. Ni neno linaloonyesha maana inayokinzana na maana ya neno asilia.
2. (a) amani
(b) mwanafunzi
(c) Tajiri
(d) mzee
3. vita-amani, mzee-kijana, maskini-tajiri, mwalimu-mwanafunzi
4. (a) **Kijana maskini** alihama jana **mchana**.
(b) **Ajuza**/ **bikizee** huyu ni mkarimu sana.
(c) **Wazee** wachache walipata usaidizi.
(d) **Mwoga** huzawidiwa.
(e) **Halali** haifai.
(f) **Tajiri mzee** wa **maskini**.
5. (a) vita, amani
(b) kijana, mzee
(c) usiku-mchana, giza-mwangaza
(d) kaskazini, kusini
(e) njaa, shibe
6. Sentensi zako zitumie vinyume hivi:
(a) tajiri
(b) furaha
(c) wepesi
(d) baridi
(e) mnuno
7. (a) utamu
(b) huzuni
(c) ardhi
(d) halali
(e) ujinga

II. Vinyume vya vivumishi.
1. (a) -nene (b) -baya (c) -eupe (d) -fupi (e) -nono (f) -chachu/-chungu/ kali?
2. wazuri-wabaya, chungu-tamu, -refu- -fupi, -nene - -konde, -eupe - -eusi
3. (a) warefu, wafupi (b) wachache, wengi (c) jeupe, jeusi (d) zuri, baya (e) tamu, chungu
4. Sentensi zako zitumie vinyume hivi:

(a)karaha
(b) -choyo (c) -chungu (d) -zuri (e) –baya

Shughuli jumuishi
1. (a) Mungu-binadamu, Mungu-shetani, raha-karaha, uzembe-bidii, uchoyo-ukarimu, uadui-urafiki, utajiri-umaskini, amani-vita, afya-magonjwa,
(b) warefu-wafupi, wembamba-wanene, marefu-mafupi, mabaya-mazuri,
2. (a) Taja nomino kama vile: darasa
(b) Taja vivumishi kama vile: kubwa-dogo

Dijitika
(a) Tumia kifaa cha kidijitali kufanya zoezi hili.
(b) Wasambazie wenzako kazi yako ili wakupe maoni yao.

Nje ya darasa
1. Taja vinyume kama vile kirefu-kifupi, mwalimu-mwanafunzi
2. Fanya zoezi hili ulivyoagizwa. Unaweza kuandika matokeo ya utafiti wako kwenye kifaa cha kidijitali au daftarini.

Shughuli ya 11:
I. Kauli ya kutenda
1. imba, ameketi, tunaandika, fanya, nunua, nuna, nung'unika, tandika, pita, furahi, samehe
2. (a) anasoma
(b) amefyeka
(c) walipita, walioufanya
(d) ninashona
(e) amevaa,inapendeza
3. (a) kataa
(b) fahamu
(c) kimbia
(d) endesha
(e) linda
4. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Mimi ninaandika kitabu.
(b) Wanafunzi hulala mapema.
(c) Mtoto alikunywa maziwa.
(d) Kabibi hapendi kufagia nyumba.
(e) Twiga wawili wanacheza kando ya mti.
5. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika aya. Aya ihusu majukumu ya watoto.

II.Kauli ya kutendea
1. tolea, letea, somea, pitia, patia, tobolea, kashifia, angulia

2. (a) amenichotea
(b) alimkimbilia
(c) akawapakulia
(d) aliwafukuzia
(e) amenipimia
3. (a) angukia
(b) angalilia
(c) chorea
(d) ongelea
(e) abiria
4. (a) Mti umeangukia nyumba.
(b) Rais amempongezea utu wake.
(c) Njeri amemwandikia Onyango barua.
(d) Watoto wanamtandikia nyanya kitanda.
(e) Chui anawawindia watoto wake.
5. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Shibli anachezea mpira.
(b) Kwaya ilimwimbia mgeni wetu.
(c) Wajukuu walimlimia babu shamba lake.
(d) Mwenyeji alimtolea mgeni mizigo yake nje.
(e) Baba alimwingilia mototo wake kwenye uwanja kuchukua mpira wake.
6. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika aya. Aya ihusu majukumu ya watoto.

III. Kauli ya kutendwa

1. chotwa, chomwa, ombwa, andikwa, tunzwa, chemshwa, thaminiwa, fugwa, lindwa
2. (a) yalichotwa (b) wamepokelewa (c) iliyopikwa,(* iliyookwa)imekatwa (d) imepangwa
(e) litang'olewa (e) wameanguliwa
3. (a) tolewa (b) hifadhiwa (c) sukumwa (d) tambaliwa (e) kaliwa
4. (a) Ugali umepikwa na Fatuma.
(b) Mpira umedakwa na golikipa.
(c) Kitabu kimeandikwa na mtoto.
(d) Asna ametembelewa na Kairo.
(e) Ubao umeandikwa na mwalimu.
5. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Nyumba hii imehamwa jana.
(b) Wimbo umeimbwa tena.
(c) Maji yalichotwa mtungini.
(d) Nyasi ndefu zitafyekwa kesho.
(e) Ngombe wote hukamwa asubuhi.
6. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika aya. Aya ihusu majukumu ya watoto.

Dijitika

1. Tumia kifaa cha kidijitali kupiga chapa.

2. (a), (b), (c) Siku za wikendi sisi kama watoto waadilifu, huwasaidia wazazi wetu kufanya kazi. Dada yangu mkubwa huhakikisha nyumba *imepigwa* deki naye Gesore hukama ng'ombe. Mimi **huwajibikia** kupika chai. Chai *hunywewa* kwa mahamri ambayo *hupikwa* na mama. Tumalizapo kustaftahi, sisi **huchotea** ng'ombe wetu maji kutoka kwa kisima na **kuwaletea** nyasi kutoka kwa shamba. Nyasi hizi *hukatwa* na *kuwekwa* mahali spesheli pa **kulishia** ng'ombe. Sisi hupenda *kuelekezwa* na wazazi wetu tunapotekeleza majukumu yetu.
(d) Msambazie mwalimu mtandaoni ili akupe maoni.

Nje ya darasa
1. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika aya. Aya ihusu majukumu ya watoto. Unaweza kukiandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali.
2. Hakikisha umetumia matamshi bora, sauti inayosikika na usome kwa kasi inayostahili.
3. Mwonyeshe vitenzi ulivyoelekezwa katika kifungu chako.

Shughuli ya 12:
Aina za sentensi:Sentensi sahili na sentensi ambatano
1. (a) Soma vifungu vya maneno ulivyopewa kwa ufasaha.
(b) (i), (iii)
(c) Vifungu hivyo vinawasilisha wazo ambalo limekamilika kimaana.

Sentensi sahili
1. Rejelea uk 141. Ni sentensi iliyo na wazo moja tu.
2. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
Barakoa zilikinga dhidi ya viini vya Korona.
Ugonjwa wa malaria husambazwa na mbu.
Ugonjwa wa kifua kikuu una tiba.
Maradhi ya UKIMWI yalimdhoofisha kiafya.
Maelfu waliangamia kutokana na maradhi ya Ebola.
3. (a), (b), (c)
4. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Ugonjwa huo umepata tiba.
(b) Maambukizi yameweza kudhibitiwa.
(c) Magugu yamesambaa shambani kote.
(d) Mbu wameeneza maradhi.
(e) Mgonjwa alipata matibabu haraka.
(f) Afya njema ina faida tele.

II. Sentensi ambatano
1. Rejelea uk 142. Ni sentensi iliyo na sentensi sahili mbili ambazo zimeunganishwa na kiunganishi.
2. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
Ugonjwa ulikurupuka na wananchi wakachanjwa.

Watoto walioambukizwa ukambi wamepata matibabu.
3. (b)
4. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Mifano:
(a) Ugonjwa huo umepata tiba lakini watu hawajikingi.
(b) Maambukizi yameweza kudhibitiwa ila chanjo zaidi zinahitajika.
(c) Magugu yamesambaa shambani kote kwani hakujalimwa.
(d) Mbu wameeneza maradhi ya malaria ingawa watu wanatumia vyandarua.
(e) Mgonjwa alipata matibabu haraka licha ya kulemewa.
(f) Afya njema ina faida tele na watu wanafaa waitunze.

Shughuli jumuishi
1. Sentensi sahili- (a), (d), (e), (f), (h), (i)
Sentensi ambatano- (b), (c), (g), (j)
2. (a) Soma kifungu ulichopewa kwa ufasaha.
(b) Yakobo alihisi maumivu mwilini.
Alihitaji kumwona daktari.
Alitumai angetibiwa haraka.
Daktari alikagua damu ya Yakobo maabarani.
Ugonjwa ulitambuliwa.
(c) Kichwa kilikuwa kinamuuma na alikuwa na joto jingi mwilini.
Alipanda gari, akalipa nauli na gari likampeleka hadi hospitalini.
Foleni ilikuwa ndefu lakini madaktari walikuwa wengi.
Yakobo alipewa dawa kisha akaruhusiwa kurudi nyumbani.
3. (a) Nywele zake zilisukwa vizuri **na** anakaa maridadi.
(b) Nyairo aliumwa na mbu **na//kwa sababu/kwa hivyo** amepata malaria.
(c) Maji yalichotwa mtoni **lakini/ila/ingawa** hayajatosha.
(d) Mtoto hajapewa chanjo **lakini/ila/ingawa** hajapata ugonjwa.
(e) Kiberiti kipya kimenunuliwa **lakini/ila/ingawa** moto haujawaka.
4. (a) Nyuzi zilinunuliwa. Nyuzi zilitumika kutengeneza kitambaa.
(b) Mahindi yamevunwa leo. Mahindi yatauzwa wiki ijayo.
(c) Nyumba hiyo imekamilika. Haijapakwa rangi.
(d) Sinywi chai. Sili vitumbua.
(e) Chakula hakijapikwa. Wageni hawajafika.

Nje ya darasa
1. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Sentensi ziwe sahili pekee. Unaweza kuziandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali kwa marejeleo ya baadaye.
2. Zingatia uakifishaji na upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Sentensi ziwe ambatano pekee. Unaweza kuziandikadaftarini au kwenye kifaa cha kidijitali kwa marejeleo ya baadaye.
3. Wasomee wenzako darasani sentensi zako wazitolee maoni.

Shughuli ya 13:
I. Ukanushaji wa wakati uliopita

1. (b), (c), (d)
2. (a) “Mizozo baina ya jamii haikufaa kutatuliwa,” Kadhi aliwashauri waumini.
(b) Alipofika hawakuwa wameondka.
(c) Je, hukuwa katika kikosi kilichoshinda mechi hiyo?
(d) Hamkuchelewa kufika darasani.
(e) Hatukufanya bidii ili tusifaulu sote.(*utafiti zaidi kuhusu mantiki katika kukanusha kitenzi cha pili)
3. (a) hakuwa (b) hawakusuluhisha (c) hakumpongeza (d) hazikufungwa (e) hakikupikiwa
4. (a) Hatukumsikiliza mwalimu wetu kwa makini.
(b) Sikuwakumbusha umuhimu wa kusameheana.
(c) Gavana hakuwataka waishi kwa amani.
(d) Hamkuombwa mdumishe amani.
(e) Hukutakiwa kufika bila kuchelewa.
5. (a) Hakikisha umetumia kiambishi –li- cha wakati uliopita. Mfano:
Sote tulienda kanisani.
(c)Rejelea uk 144 kupata vikanushi vya kila nafsi kisha ukanushe sentensi zako. Mfano:
Sote hatukuenda kanisani.

II. Ukanushaji wa wakati uliopo

1. (b), (c), (d), (e)
2. (a) Wananchi hawaendelei kufurika uwanjani.
(b) Wewe huchezi na moto.
(c) Sijuti kwa kitendo hicho.
(d) Hamcheki kwa nini?
(e) Waumini hawaelekei kanisani.
3. (a) haidumishwi
(b) hapeperushi
(c) hawachungi
(d) haliendi
(e) hampaswi
4. (a) Sishangai kwamba mvua hainyeshi asubuhi.
(b) Hawahudhurii mkutano wa amani.
(c) Hutakiwi kutii sharia za shule yako.
(d) Triza hasafiri kuelekea nyumbani.
(e) Hamchimbi mitaro ya kupanda miti?
5. (a) Hakikisha sentensi zako zina kiambishi –na- cha wakati uliopo. Mifano:
Wanafunzi wanafunzwa kuhusu manufaa ya kuishi kwa amani.
Chifu anasuluhisha mzozo baina ya wanakijiji.
(b) Rejelea ukurasa 146 kupata jinsi nafsi zinabadilika katika ukanushaji ili uweze kukanusha sentensi zako.Mifano:
Wanafunzi hawafunzwi kuhusu manufaa ya kuishi kwa amani.
Chifu hasuluhishi mzozoz baina ya wanakijiji.

III. Ukanushaji wa wakati ujao.

1. (a), (c), (d), (e)
2. pigia mstari maneno yafuatayo:
(a) haitachezewa (b) haitaruhusiwa (c) hawataruhusiwa(d) sitaunga (e) haitatuletea
3. (a) Je, hamtaacha kuzozana?
(b) Sitatarajia kushinda mbio za nyika.
(c) Hutamtunza mtoto huyo kama wako.
(d) Mpira usipopigwa kwa nguvu hautatoka nje.
(e) Kwao hakutapendeza kwa kupandwa miti aina mbalimbali.
4. (a) Hakikisha sentensi zako zina kiambishi –ta- cha wakati ujao. Mifano:
Mizozo yote itatatuliwa.
Baba mkwe atawapatanisha wanawe baada ya zogo hilo la mashemeji.
(b) Rejelea ukurasa 147 kupata jinsi nafsi zinabadilika katika ukanushaji ili uweze kukanusha sentensi zako.
Mifano:
Mizozo yote haitatatuliwa.
Baba mkwe hatawapatanisha wanawe baada ya zogo hilo la mashemeji.

Shughuli jumuishi
(a)

Wakati uliopita	Wakati uliopo	Wakati ujao
nilifikiri, ilikuwepo,	ninaanza, linaloweza, wanapoishi, wanaelewana, panatokea, anastahili, wanaozozana, unahitajika, inakua	sitawahi, utapata, itakuwepo, nitajizatiti, nitausuluhisha, nitakuwa

(b) Tunga sentensi sahihi kwa kila kitenzi ulichotambua.
(c) Kanusha sentensi hizo ifaavyo. Zingatia ukanushaji wa kila nyakati.
(d) Sambaza kazi yako kwa wenzako mtandaoni ili wakupe maoni yao.

Dijitika
1. Tunga sentensi zilizokanushwa kama ulivyoagizwa. Zingatia nyakati zote. Mifano:
Wakati uliopita-Kituo cha polisi hakikuwekwa mpakani.
Wakati uliopo- Jamii zetu hazina ugomvi tena.
Wakati ujao- Kizazi hiki hakitaki ugomvi.
2. Sambaza kazi yako kwa wenzako mtandaoni.

Nje ya darasa
1. Tunga sentensi zilizokanushwa kama ulivyoagizwa. Zingatia nyakati zote.
2. Msomee mzazi au mlezi sentensi hizo ulivyoagizwa. Zingatia usomaji kwa ufasaha.

Shughuli ya 14:
Ukubwa wa nomino
1. (a) darasa, dawati, mlango, kitabu

(b) jidarasa, jidawati, lango/jilango, jitabu
2. lango, kono, jitu, buzi, vulana
3. (a)
4. (a) jana
(b) jike
(c) lango/jilango
(d) jisichana/sichana
(e) jibarabara
5. majumba, jitabu, jiduka,jijini, jitu, jigari
6. (a) Jizee lenye jishamba kubwa limehama.
(b) Majisichana yaliyokosa adabu yaliadhibiwa na jimama lile.
(c) Jigari lililoligonga jivulana lile limepelekwa kituoni.
(d) Gonjwa la UKIMWI limeathiri majitu mengi.
7. (a) ji-meza
(b) ji-ti
(c) ji-gari
8. (a) Jitu lenye jumba lile limehama.
(b) Majana makubwa yamechaguliwa kujiunga na jeshi.
(c) Janajike lenye kono kubwa lililikaba na kuliinua jizi.
(d) Majigari makuukuu yatauzwa.
9. mtoto-toto, kitabu-jitabu, sahani-jisahani, mti-jiti, njia-jia
10. (a) Tunga sentensi ulivyoagizwa. Hakikisha nomino ziko katika ukubwa. Sentensi zenyewe zihusu matumizi ya pesa. Mfano:
Jitajiri lilinunua jigari hili.
(b) Ziwasilishe ulivyoelekezwa ili wenzako wazitathmini.

Nje ya darasa
(a) Mifano: kijiko, kikombe, meza, sufuria
(b) Mfano:

Nomino(wastani)	**Ukubwa**	
	umoja	**wingi**
kijiko	jijiko	Majijiko

(c) Msomee mzazi au mlezi ulicyagizwa.
(d) Tunga sentensi ulivyoagizwa. Hakikisha umezingatia sarufi katika utunzi wako.

Shughuli ya 15:
I. Usemi halisi
1. (a) Rejelea uk 150 kwa maelezo zaidi. Ni nukuu ya maneno halisi yaliyosemwa na mnenaji bila kuongeza au kutoa lolote.
(b) Unaweza kuziandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali kwa matumizi ya baadaye.
Mfano:
"Nenda sokoni," mama aliagiza.
Mwalimu alisema,"Nimechoka tiki baada ya kufanya kazi mchana kutwa!"
(c) Sambaza kazi yako kwa wenzako ili wakupe maoni yao.

2. (a) Tumia kifaa cha kidijitali au vitabu vya ziada kufanya zoezi hili. Kifungu kihusu maadili ya mtu binafsi.
(b) Unaweza kuzidondoa na kuzinakili mahali kwa matumizi ya baadaye.
3. (a), (b)

II. Usemi wa taarifa.
1. (a) Rejelea uk 150-151 kwa maelezo zaidi. Ni ripoti ya maneno yaliyosemwa na mtu bila kutumia alama za kunukuu wala kubadili ujumbe asilia.
(b) Unaweza kuziandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali kwa matumizi ya baadaye.
Mifano:
Mama alimwagiza aende sokoni.
Mwalimu alisema kuwa alikuwa amechoka tiki baada ya kufanya kazi mchana kutwa.
(c) Sambaza kazi yako kwa wenzako ili wakupe maoni yao.
2. (a) Tumia kifaa cha kidijitali au vitabu vya ziada kufanya zoezi hili. Kifungu kihusu maadili ya mtu binafsi.
(b) Unaweza kuzidondoa na kuzinakili mahali kwa matumizi ya baadaye.

Shughuli jumuishi
1. (a) Mwalimu alisema kuwa hangechelewa kufika darasani.
(b) Mgeni alimwambia mzazi kuwa ikiwa wangetia bidii wangefaulu.
(c) Kachero alimuuliza/alitaka kujua sababu yake ya kueneza uvumi.
(d) Mshauri aliwaambia wanafunzi wasiwanyanyase wenzao wa jinsia tofauti.
(e) Mtoto alijibu kuwa siku ambayo ingefuata ingekuwa Jumamosi.
(f) Mama alisema kuwa angesafiri jioni ya siku ambayo ingefuata.
(g) Naomi alimuuliza Jane ikiwa yeye alikuwa mkulima wa pareto.
(h) Kasisi aliwaonya watubu dhambi zao au wakose utukufu wa Mungu.
2. (a) “Nipe leseni zote,” mwelekezaji aliomba.
(b) “Huenda mvua ya masika itanyesha kuanzia kesho,” mtabiri wa hali ya hewa alitabiri.
(c) “Tutacheza kwa bidii ili kuibuka na ushindi,” wachezaji walisema.
(d) “Lo! Wananchi wanakunywa maji ambayo hayajatiwa dawa ya kuua viini hatari!’ Afisa wa afya alishangaa.
(e) “Wazee ni wangapi katika eneo bunge hili langu?” Mbunge aliuliza.
(f) “Wewe, toka hapa!” Aliamrishwa.
(g) “Soko la mazao yenu liko tayari,” wakulima waliambiwa.
(h) “Nimewasili na darasa bado linafagiliwa,”alijisemea.(*Mwalimu alishangaa kuwa bado darasa lilikuwa linafagiliwa alipowasili)
3. (a) Andika sentensi hizo kwenye kifaa cha kidijitali au kwenye daftari.
(b) Zibadilishe ulivyoagizwa. Rejelea uk 151 kwa maelezo zaidi.

Nje ya darasa
1. (a) Andika sentensi hizo kwenye kifaa cha kidijitali au kwenye daftari.
(b) Zingatia kusoma kwa ufasaha katika zoezi hili.
(c) Angalia ikiwa sentensi zinazingatia sarufi na sharia za uandishi wa usemi halisi na usemi wa taarifa.

Tathmini ya 1
Sehemu ya A
Zoezi la 1 – Mazungumzo ya ana kwa ana
(a) Usafi wa kibinafsi ni usafi unaomhusu mtu mwenyewe. Mtu anafaa kuhakikisha kuwa mwili wake na nguo zake ni safi kila wakati. Akifanya hivi, hatatoa harufu mbaya isiyopendeza wanaokaa karibu naye.
(b) kuoga mwili angalau mara moja kwa siku, kupiga mswaki baada ya kuamka na kabla ya kulala, kuchana nywele ili ziwe nadhifu, kukata kucha ndefu, kunawa mikono kabla ya kula na baada ya kutoka msalani, kufua sare za shule,n.k
(c) mdomo wake utatoa harufu isiyopendeza, wenzake watamwambaa na kumtenga kwa sababu ya harufu hiyo, meno yatakuwa dhaifu, atapata magonjwa kama vile jino/meno kuuma
(d) Kwanza nitayatoa na kutandika mengine safi iwapo yapo. Kisha nitafua yale malazi chafu na kuyaanika kwenye jua ili yakauke. Baada ya kukauka, iwapo sikutandika malazi mengine, nitatandika kitanda changu na hayo ambayo nilifua.

Zoezi la 2 Ufahamu wa kusikiliza
Kifungu kisomwe mara mbili. Mwanafunzi anayejibu maswali afahamu kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara mbili.
(a) misitu, udongo
(b) husaidia kusafisha hewa, huzuia mmomonyoko wa udongo, huwa makazi ya baadhi ya wanyama kama vile tumbili, baadhi huwa lishe kwa binadamu na wanyama.
(c) kutatokea mmomonyoko wa udongo.
(d) mahali pa kuishi/maskani/makao/mastakimu

Zoezi la 3 Kusoma kwa sauti
Mwanafunzi anayesoma apewe nakala kwanza ili ajitayarishe.
(a) Rekodi ya idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa dakika moja inahitajika.
(b) Onyesha kwa mshazari (/) mahali mwanafunzi anapofikia kusoma dakika moja ikiisha.
(c) Anayesoma aruhusiwe asome hadi mwisho wa kifungu.
(d) Pigia mstari maneno yote ambayo mwanafunzi anatatizika kuyasoma na kuyatamka vizuri.
(e) Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi anaweza kusoma kwa usahihi chini ya dakika moja.

Sehemu ya B
Zoezi la 1 Ufahamu wa kusoma
(a) kuwaonyesha upendo
kuwasaidia kujua kuliko misala, bwalo na mabweni
kuwajuvya kuhusu ratiba ya shule
(b)kufuata sheria za shule, kuwasahuri watovu wa nidhamu, kuwaripoti watovu wa nidhamu kwa mwalimu ili wapewe ushauri zaidi,kuwasaidia wenzao wakiumia katika michezo kwa kuwapa huduma ya kwanza,kuhakikisha mazingira ya shule ni safi,kuwasaidia na kuwashirikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum,

(c) kuibia wanafunzi na walimu, kulangua dawa za kulevya, kutumia dawa za kulevya, kuchokoza wanafunzi wengine, kutusi wengine, kutovaa sare ya shule bila sababu, kukosa kufanya kazi ya ziada, kukosa kusikiliza na kufuata ushauri mzuri wa walimu na wanafunzi wengine,kuchafua mazingira,n.k
(d) kuwahusisha

Zoezi la 2 – Ufupisho (*kwenye matini asilia ni 'Ufahamu wa kusikiliza)uk 155
(a) Kila binadamu,wa kike kwa kiume, ana hisia na ana uhuru wa kuwasilisha hisia zake kwa njia yoyote ile .
(b) Jinsia zote zinafaa kuzumbua riziki.
(c) Jinsia ya kike inatetewa sana huku ya kiume ikitengwa. Jinsia zote zinafaa kuhudumiwa kwa njia sawa.
(d) Tuzingatie usawa/ Usawa wa kijinsia

Sehemu ya C
Kuandika
(a) hii ni barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko.
(b) barua iwe na sehemu hizi: anwani ya anayeandika, tarehe ya kuandika, mtajo, utangulizi, mwili na hitimisho.
(c) aya ya kwanza ihusishe salamu na kujulia rafiki hali.
(d) lengo la barua lijitokeze kuanzia aya ya 2 hadi ya pili kutoka mwisho.
(e) aya ya mwisho ihusishe kutuma salamu kwa wapendwa na matarajio ya mwandishi.
(f) lugha iwe inayoeleweka kwa urahisi.

Sehemu ya D
Sarufi
1. B 2. C 3. A 4. D 5. A
6. malezi
7. Mvua nyingi itanyesha.
8. lilikuwa 9. a, ya 10. Mahali pachafu patasafishwa tena.
11. Juma alimtembelea Natasha.
12. Watu wengi walienda hospitalini.
Wauguzi waliwahudumia.
13. Maria hatatuma kazi ya ziada kwa baruapepe.
14. gombe/jigombe
15. Mosenya aliwahimiza kuwa walifaa kuzingatia maadili kwa kila jambo lililolifanya.

Sehemu ya E
Zoezi la 1 - Fasihi
(a) wimbo wa watoto/chekechea
(b) huwa fupi, baadhi ya vifungu hurudiwarudiwa
(c) wanacheza, wanakimbia kwa baba kumsaidia
(d) watoto, mama, ng'ombe
(e) Ni vyema kuwasaidia watu wanapopata changamoto.

Zoezi la 2 – Novela

Majibu katika zoezi hili yanategemea novela ambayo mwanafunzi ameisoma. Mwanafunzi anaweza kuambatisha hoja na mfano kutoka kwa kazi ya fasihi aliyoisoma.

(a) Mifano ya maudhui: tamaa na ubinafsi, ukatili, utu, uongozi, kazi, bidii, kuwajibika, malezi

(b) Mifano ya mandhari: mandhari ya wakati, mandhari ya mahali na mandhari ya hali

(c) Mhusika anaweza kuwa na sifa kama vile: karimu, mwongo, mwajibikaji, katili, mwenye utu, mwenye msimamo thabiti.

Sifa hutegemea mhusika anavyotenda, anavyonena, anavyosemwa na wahusika wengine au mwandishi.

(d) Mifano ya mbinu za lugha: kinaya, tashbihi, takriri, mbinu rejeshi, tashihisi, nidaa

Tathmini ya pili

Sehemu ya A

Zoezi la 1(a) mazungumzo ya ana kwa ana

1. Usafi wa kibinafsi ni usafi unaomhusu mtu mwenyewe. Mtu anafaa kuhakikisha kuwa mwili wake na nguo zake ni safi kila wakati. Akifanya hivi, hatatoa harufu mbaya isiyopendeza wanaokaa karibu naye.

2. Mimi huoga mwili angalau mara moja kwa siku, ninapiga mswaki baada ya kuamka na kabla ya kulala, ninachana nywele ili ziwe nadhifu, ninakata kucha ndefu, ninanawa mikono kabla ya kula na baada ya kutoka msalani na kufua sare zangu za shule

3. Mwili huwa safi, anapata ujasiri wa kutangamana na watu, afya inakuwa bora, mwili hautoi harufu isiyostahili.

4. Mdomo wa mtu hutoa harufu isiyopendeza, wenzake watamwambaa na kumtenga kwa sababu ya harufu hiyo, magonjwa yanaweza kumwandama, mwili wake unakuwa maskani ya wadudu kama vile chawa na funza,mja hukosa ujasiri wa kutangamana na wengine,

5. Nitamshawishi kwa kumweleza manufaa ya kuzingatia usafi wa kibinafsi.
Nitamwonyesha kwa vitendo namna ya kudumisha usafi.

Zoezi la 1(b) - Ufahamu wa kusikiliza

6. Walibishania barabara ya kwenda kidimbwini, waligombania matumizi ya kidimbwi hicho, walichukiana kwa sababu ya matunda yaliyokuwa msituni, kulikuwa na mzozo kuhusu mpaka uliotenganisha ardhi zao

7. Mimea kunyauka na wanyama kukonda, maji yaliyotegemewa kidmbwini kukauka,chakula chote kuisha,mashamba kugeuka jangwa, wanyama na binadamu kukosa matumaini

8.Fisi alitaka binadamu afukuzwe na hali hii ingeleta vita na amani ingekosekana.

9. Uhasama baina yao ungeendelea.
Ng'ombe kondoo na mbuzi bado wangekuwa wanaishi msituni.
Binadamu asingekuwa anatunza misitu.
Wote,wanyama na binadamu,wangeendelea kuathirika na mabadiliko ya hali ya anga bila kupata suluhu

10. Njia bora ya kuonyesha upendo kwa mwenzako ni kwa kumsaidia apatapo shida. Msaada huu haufai kuzingatia uhusiano wa kijamaa. Unapomsaidia mtu ambaye hamhusiani kwa damu, huo ndio udugu wa kweli.

Zoezi la 2 Kusoma kwa sauti
Mwanafunzi anayesoma apewe nakala kwanza ili ajitayarishe.
(a) Rekodi ya idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa dakika moja inahitajika.
(b) Onyesha kwa mshazari (/) mahali mwanafunzi anapofikia kusoma dakika moja ikiisha.
(c) Anayesoma aruhusiwe asome hadi mwisho wa kifungu.
(d) Pigia mstari maneno yote ambayo mwanafunzi anatatizika kuyasoma na kuyatamka vizuri.
(e) Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi anaweza kusoma kwa usahihi chini ya dakika moja.

Sehemu ya B
Zoezi la 3(a) - Ufahamu wa kusoma
1. Nyaramba ni kijana mtiifu kwa kuwa yeye humheshimu kila mja pasipo kujali umri wala cheo.
2. Anapotumwa na wakuu wake, yeye huenda shoti
Alimfahamisha muuzaji kuwa alikuwa amemrejeshea hela zaidi ya alivyopaswa.
3. Angepotoka kimaadili, muuzaji angepata hasara, muuzaji angegundua baadaye na labda aanze kumsaka au hata kumchukulia hatua ya kisheria
4. Ukiwahini wengine mali au vitu vyao, hata nawe utahiniwa vivyo hivyo na wengine.

Zoezi la 3(b) Kifungu cha ufahamu
5. Uamuzi wa Mwenyezi Mungu.
6. B
7. Ukosefu wa utu utaendelea kushamiri, watoto wataendelea kuibwa na kulanguliwa.
8. B

Sehemu ya C- Kuandika
Hii ni insha ya maelekezo
1. Hatua zifuatane kimantiki moja baada ya nyingine.
2. Maelezo yawe yanaeleweka.
3. Lugha rahisi inayoeleweka kwa urahisi itumike.
4. Mbinu za lugha kama vile tashhisi zisitumike kwani hapa ni maelekezo ndio muhimu.
5. Mwanafunzi azingatie uakifishaji na sarufi katika insha yake.

Sehemu ya D Sarufi
1. B 2. D 3. C 4. B 5. D 6. ruka 7. ndiye/ni
8. u, ya 9. Mkunga hamhudumii mama mjamzito.
10. KI-VI – ki, LI-YA – li
11. “Daudi, kuwa mwanafunzi mwenye adabu,” mwalimu alimwambia.
12. (a) choyo (b) kijana/mchanga

13. Chakula kitamu kiliandaliwa na mwenyeji kwa ajili ya wageni wake.
14. Bao maridadi lilifungwa na mshambuliaji.
15. kombe/jikombe mfano: Kombe lilijazwa uji.

Sehemu ya E
Zoezi la 1 - Fasihi
(a) wimbo wa kazi(hodiya)
(b) huimbwa katika mazingira ya kazi, humbwa na wanaofanya kazi fulani, hutofautiana kulingana na kazi inayofanywa
(c) wanafanya kazi ya kukata kitu fulani kama vile gogo au mti.
(d) uradidi/takriri
(e) wimbo huu huhimiza bidii – hapa ndio riziki
Huhimiza kutokata tamaa – kata usichoke

Zoezi la 2 Novela
Majibu katika zoezi hili yanategemea kazi ya fasihi ambayo mwanafunzi ameisoma. Mwanafunzi anaweza kuambatisha hoja na mfano kutoka kwa kazi ya fasihi aliyoisoma.
(a) Mifano ya maudhui: tamaa na ubinafsi, ukatili, utu, uongozi, kazi, bidii, kuwajibika, malezi
(b) Dhamira ni lengo la mwandishi. Mifano ya dhamira: kuonya, kuelimisha, kuburudisha, kukashifu tabia fulani, kuelekeza
(c) Mifano: umuhimu wa elimu, umuhimu wa teknolojia, umuhimu wa maadili kwa mtu binafsi, madhara ya matumizi ya dawa za kulevya